KITABU CHA MWONGOZO KATIKA

# KUANZISHA MAKANISA MAPYA



na *Harold Cummins*

## MIPANGO KUMI INAYOWEZA KUSAIDIA

# KITABU CHA MWONGOZO KATIKA



na *Harold Cummins*

KITABU CHA MWONGOZO KATIKA

# KUANZISHA MAKANISA MAPYA

# KUANZISHA MAKANISA MAPYA

*Na*

***Harold Cummins***

Kutumiwa kama:
Somo la kibinafsi la jinsi ya kuanzisha makanisa mapya
au
Kitabu cha mwongozo kutumika na makundi yakikutanika kujifunza jinsi ya kuanzisha makanisa mapya

Picha Zimechorwa na Phil Lasse

*Copyright 1981*
*Baptist Publications House,*
*P.O. Box 30370*
*NAIROBI, KENYA*

***Jointly published by:***
***Baptist Publications House and Evangel Publishing House***

**Printed by**
**Baptist Publications House**
**P.O. Box 30370**
**Nairobi, Kenya**

# YALIYOMO


UTANGULIZI .................................. 7

I. MPANGO MAALUM WA KIMSINGI ...... 11

II. MIPANGO MINGINE KWA KUANZISHA MAKANISA. .............................. 36

A. Mpango wa Kutumia Vikundi ........... 40

B. Mpango wa Kusoma Maandiko Matakatifu 46

C. Mpango wa Kikundi cha Urafiki ......... 50

III. MIPANGO MIFUPI YA KUANZISHA MAKANISA MAPYA. ...................... 55

A. Kuanzisha Makanisa na Muziki ......... 55

B. Kuanzisha Makanisa na Wanafunzi ...... 56

C. Kuanzisha Makanisa na Maombi ........ 58

D. Kuanzisha Makanisa na Ramani ......... 60

E. Kuanzisha Makanisa na Maonyesho ...... 62

F. Kuanzisha Makanisa na Kaseti .......... 64

MWISHO "Moto Wako Uje!" ...................... 65

NYONGEZA: Kazi Kufanyika Kusaidia Kujifunza .... 67

# UTANGULIZI

Viongozi wengi wa makanisa wameanza kugundua furaha ipatikanayo katika kuanzisha makanisa mapya. Je, wewe umewahi kuwa na furaha hiyo? Kitabu hiki kinaweza kuwa mwongozo wako mzuri uanzishapo makanisa pia. Wakati utakapokuwa ukisoma, utajifunza mawazo mapya ya uanzishaji na uendelezaji wa makanisa. Katika kitabu hiki kuna mipango kumi kutumia unapoanzisha makanisa.

Baadhi ya maendeleo muhimu yaliyomo ufalme wa Mungu, yameonekana katika kuanzisha kwa makanisa mapya. Kwa vile idadi ya watu ulimwenguni inaongezeka, pia makanisa yanahitaji kuongezeka. Hivyo, Mungu anakualika uingie katika ile furaha ya mpango wake wa uinjilisti wa ulimwengu na uanzishaji wa makanisa.

Habari zimeanza kusikika kutoka sehemu mbalimbali za dunia, zikieleza juu ya makanisa mapya mengi yanayoanzishwa. Katika wilaya moja ya Kenya, makanisa yaliongezeka kutoka matano hadi sitini na tano katika muda chini ya miaka minane. Viongozi wa makanisa ya wilaya hiyo wamejitoa kufuata mpango wa Agano Jipya kuwa "Wavuvi wa watu....wajumbe wa Kristo....wafanya kazi wa Mungu.... wavunaji....kuongezea kanisa kila siku....kulijenga kanisa."

Mfanya kazi mmoja aliyefanya kiwandani, alitaka sana kumtii Kristo. Aliishi katika eneo ambapo dini ya kienyeji ilikuwa na nguvu sana. Lakini katika Biblia yake, alisoma juu ya "kutupa wavu wake....kuwafanya watu wawe wafuasi....kuzaa matunda mengi." Hivyo alianza kutembelea nyumba kwa nyumba, kijiji kwa kijiji akizungumza na watu juu ya Kristo. Alisimulia hadithi za Biblia na kuwakaribisha watu watubu na kumpokea Kristo. Baada ya majuma

machache, kanisa lilianzishwa na wale waliotubu na kuamini. Leo, kuna makanisa tisa katika eneo hilo. Mungu alitoa mibaraka mingi ya ajabu wakati Wakristo wale walipojaribu kuwa waaminifu kuvuta watu wengine....jamaa nyingine....na vijiji vingine kwa Kristo.

Mwalimu mmoja hapa Afrika alikuwa na upendo mkuu kwa watu. Alipanga mpango wa kutumia vikundi maalum kuanzisha makanisa mapya. Kwa njia hii, zaidi ya watu 3,000 waliokolewa na kubatizwa. Pamoja na hayo, zaidi ya makanisa mapya 50 yalianzishwa. Mwalimu huyo amejitolea kazi hiyo tu ya uanzishaji wa makanisa na uelimishaji wa viongozi. Mwalimu huyo anaamini kwamba **kukua** ni kazi ya kwanza na ya muhimu kuliko kazi zote za kanisa.

Taarifa hizi ni za kufurahisha sana. Mungu anawapa watu wake Roho wake, vipawa vyake, na mibaraka yake. Lakini, labda ungependa kuuliza: "Hivi kuna njia rahisi ambayo naweza kuitumia kuanzisha kanisa?" Ndiyo, tena siyo njia moja tu, zipo njia nyingi za kuanzisha makanisa. Kwanza kitabu hiki kitakupa mpango moja maalum ambao ni msingi wa mipango yote. Kisha, utakapoendelea kukisoma, utasoma habari ya mipango na njia nyingine. Chagua mpango utakaofaa kulingana na mazingira na hali yako. Fuata mpango huo kwa uangalifu; ubadilishe tu, pale hali ya mazingira itakapokulazimisha uibadilishe.

Kwa nini imetubidi tuanzishe makanisa mapya? Biblia imejaa na sababu nyingi. "Kristo alilipenda **kanisa** akajitoa kwa ajili yake." (Waefeso 5:25). Kanisa ni mpango wa Kristo wa kujipatia wafuasi, kufundisha imani, na kuvuta ulimwengu wote. Kristo alisema, "Nitalijenga kanisa langu." Tumebahatika sana kukaribishwa kuungana na Kristo katika kutenda kazi yake Mungu.

Mungu hupenda kwamba watu wengi zaidi wapate kuwa waamini. Mungu hutumia makanisa kuwavuta waamini wengi zaidi. Mungu hutumia makanisa kuyabadilisha maisha ya

watu. Makanisa mengi, mamia kwa mamia, yanahitajika ili kusaidia kujenga jamaa nzuri, vijiji vizuri, miji mizuri na hata mataifa mazuri.

Kanisa ni nini? Katika kitabu hiki, "kanisa" maana yake ni kundi la waamini wa kikristo ambao husali na kushirikiana katika kazi ya Mungu kufuatana na mfano uliomo Agano Jipya.


Makanisa yanaanzishwa na viongozi walio na hamu kubwa kushirikisha Habari Njema ya Kristo. Makanisa huzidishwa wakati ambapo watu zaidi na zaidi huja kwa Kristo kwa toba na imani. Ndipo hawa Wakristo wachanga huanza kuchukua hatua ile ya furaha ya ajabu, yaani, kukua katika Kristo. Waishi katika ushirika na Mungu, pamoja na kusaidiana wao kwa wao. Waamini hawa humtumikia Kristo kama mawakili na mashahidi wake. Mwishowe, kanisa jipya hili litazaliana kwa kujaribu kuanzisha kanisa jipya jingine.

Mungu hukusudia kwamba, makanisa yakue! Hivyo ndivyo Mungu hupatanisha ulimwengu naye mwenyewe na kujipatia watu ambao ni wake (II Wakorintho 5:19 na I Petro 2:9-10). Kusudi la Mungu ni kwamba vitu vyote viwe pamoja "katika Kristo" (Waefeso 1:10), na ya kuwa watu wapokee maisha mapya tele (Yohana 4:13-14). Makanisa yakuapo, Habari Njema huenezwa na kueleweka (Matendo 1:8), na lile "Kundi la Mungu" hutumikiwa (Matendo 20:28). Mambo yote haya ya kushangaza hutokea watu wanapoletwa kwa Kristo na makanisa mapya kuanzishwa.

# I
# MPANGO MAALUM WA KIMSINGI

Makanisa yataanzishwa vizuri vipi? Kitabu hiki kitakusaidia kufahamu hatua muhimu za kufuata ili kuanzisha kanisa. Ufuatao ni mpango maalum ule. Mpango maalum wa kimsingi huo unazo hatua saba:

## *HATUA SABA KATIKA KUANZISHA KANISA JIPYA*



Sasa tuchunguze hatua hizi moja moja. Soma kila hatua kwa uangalifu na kuwepo tayari kujitoa kwa Mungu kwenda na kufanya kila hatua.

## HATUA 1: OMBA NA PANGA.



Maombi yalikuwa jambo la maana sana kwake Yesu: "Hata alfajiri na mapema sana akaondoka, akatoka akaenda zake mahali pasipokuwa na watu, akaomba huko." (Marko 1:35) Aliomba alipobatizwa, kabla ya kuwaita wafuasi, kabla ya kwenda kujibu mashtaka yake, penye kifo chake, pamoja na nyakati nyingine nyingi katika maisha yake. Vivyo hivyo inatubidi sisi tuombe tukitafuta uongozi wa Mungu katika kuanzisha kanisa jipya.

Maombi ndio msingi wa kuanzisha makanisa mapya. Wafundishe washiriki wako juu ya umuhimu wa kuanzisha makanisa mapya mengine, tena uwasihi waombe nguvu ya Mungu katika kuanzisha kanisa jipya. Pia, uwasihi wazee wa kanisa na waalimu wa Shule ya Jumapili waombe kila mara ili Mungu awe kiongozi wa kazi hii muhimu.

Jambo jingine muhimu ni kupanga. Ni lazima kuomba na kupanga viende pamoja. Hii ndiyo hatua ya kwanza ya kuanzisha kanisa: **Omba na panga.** Kuna mifano ya watu wakipanga Bibliani. Soma Luka 4:18-19. Hapo, twasoma juu ya mpango wa Yesu kwa kazi yake. Katika Mathayo 9:35 twasoma ya kuwa kulikuwa na sehemu nyingi mbalimbali katika mpango wa kazi ya Yesu: Alikwenda kijiji kwa kijiji akifundisha, kuhubiri na kuponya. Mfano mwingine wa mpango katika Biblia ni lile Agizo Kuu la kuwavuta watu lililopo Mathayo 28:19-20. Huu ni mpango rasmi wa Yesu wa kueneza Habari Njema.

Watu hupanga mambo yao ili wapate matokeo mazuri ya kazi yao. Kwa mfano, mjenzi sharti apange ili aweze kujenga daraja zuri. Hupanga mambo kama: mahali, wafanya kazi, vifaa na gharama. Vile vile, mpango unahitajika katika kuanzisha kanisa jipya. Hatua sita zifuatazo zitakusaidia upangapo.

## HATUA 2: TAFUTA WASAIDIZI.



Katika Mathayo 4:17-22 tunasoma juu ya wasaidizi wanne wa Yesu. Aliwaambia wawe "wavuvi wa watu". Ingawa Yesu alikuwa na uwezo wote, hata hivyo, alitaka watu wamsaidie. Vivyo hivyo, utahitaji watu wakusaidie kuanzisha kanisa. Huwezi kufanya kazi yote peke yako.

Ikiwa Mungu anakuongoza uanzishe kanisa jipya, ungejaribu kuvuta wasaidizi wawili au watatu kukusaidia. Ni lazima wawe Wakristo wapendao wapotevu, tena watake kuwaleta kwa Kristo. Hapo chini ndiyo mambo muhimu kwa hao utakao watumiwe kama wazaidizi:

Ni lazima wawe wameokolewa kweli (II Timotheo 1:12).
Ni lazima wawe wanaishi maisha safi (Warumi 12:2).
Ni lazima wawe na nguvu ya Roho Mtakatifu (Matendo 1:8).
Ni lazima wewe na wasaidizi wako mwombe pamoja kila wakati (Marko 11:24).

Fikiria juu ya washiriki wa kanisa lako. Fikiria majina ya watu kadhaa ambao wangekuwa wasaidizi wazuri. (Muhimu: katika kazi ya kuanzisha makanisa, ni vema kuwa na wasaidizi wa namna yako - wake au waume). Hapa chini, kuna nafasi. Tumia nafasi hizo kuandika majina ya watu **unaodhani** wangefanya kazi pamoja nawe kuanzisha kanisa jipya:

1) ______________________________

2) ______________________________

3) ______________________________

4) ______________________________


Omba ya kuwa, wawili au watatu kati ya watu hawa watakubali kukusaidia. Mungu yuko tayari kukuongoza. Inakubidi kwenda kuzungumza na watu hawa juu ya umuhimu wa nafasi hii. Waambie jinsi Mungu anavyokuongoza kuanzisha makanisa mapya. Uwasihi wakusaidie kulianzisha kanisa jipya. Bila shaka, Mungu atawabariki mtakapofanya kazi pamoja.

## HATUA 3: CHUNGUZA MAENEO.

Pamoja na wasaidizi wako, tafuta maeneo mapya ambapo kanisa jipya linahitajika. Ili uchunguze vizuri, fanya mambo haya mawili:

A. **Nenda** kwa maeneo mawili au matatu, ujaribu kugundua mahali ambapo makanisa yanahitajika.

B. **Uliza** maswali kwa watu wanaoishi katika maeneo hayo.



Wewe na wasaidizi wako mtakapoingia maeneo mliyochagua, lazima mwombe Mungu awaongoze. Fikiri juu ya kijiji chako, au mji wako au wilaya yako kwa uangalifu. Baadhi ya watu wanaishi mbali na kanisa. Wasio Wakristo hawatasafiri safari ndefu kusikiliza habari za Yesu. Hata Wakristo hawapendi kusafiri sana kuhudhuria ibada. Watu hupenda kwenda kwenye kanisa lililo karibu nao. Tena watu hupenda kwenda kanisani na watu ambao wanawafahamu na kuwaona mara kwa mara. Pia, watu wengi hupenda kwenda kwenye kanisa dogo ambalo wanaweza kumtumikia Mungu kwa vipawa vyao. Kwa hivyo wewe na wasaidizi wako mwende kutafuta maeneo yanayohitaji makanisa zaidi.

Katika Mathayo 9:35, twasoma kwamba "**Yesu alikwenda**" kwa miji na vijiji vyote. Hata wewe unalazimika kwenda. Kusoma tu katika kitabu hiki namna ya kuanzisha makanisa hakutoshi. Wewe na wasaidizi wako mnalazimika kwenda katika maeneo mawili au matatu kutafuta "milango ya mahitaji" iliyo wazi. Mtakapozidi kujifunza zaidi juu ya maeneo yanayolizunguka kanisa lako, Mungu atawaongoza katika kuanzisha makanisa mapya.

Mtakapokwenda kuchunguza maeneo, tumia maswali 12 yafuatayo ya kuuliza:

1) **Watu wangapi** wanaishi katika eneo hili?
2) Wanazungumza kwa **lugha** gani?
3) Je, **kuna watu zaidi** wanaohamia hapa?
4) Ni **makanisa gani** hapa katika eneo hili?
5) Kuna **barabara, shule**, na **maduka** gani hapa?
6) **Mahitaji** ya watu wa hapa ni yapi?
7) **Viongozi** wa hapa walio muhimu ni nani?
8) Je, kuna **ndugu na marafiki** wa washiriki wetu hapa?
9) Je, kuna **mshiriki** wetu ye yote **aliyehamia** eneo hili?
10) Je, **tutawavutaje** watu kwa Kristo?
11) Je, kuna **mahali** ambapo watu wanaweza kukutana kuabudu ama kujifunza Biblia? (Nyumba, shule, duka, au jengo la kijiji).

12) Je, **tunahitaji ruhusa** kuendesha mikutano ya kidini hapo?

Itakuwa lazima kwenda kwenye maduka, nyumba na maofisi mengi kuuliza maswali haya. Hivyo tayarisha kidaftari na maswali haya. Acha nafasi ili ujaze majibu yatakayotolewa na watu.

Pengine unajiuliza, "maswali hayo yatawezaje kunisaidia?" Tutakupa sababu kuonyesha faida ya kila swali. Namba ya kila sababu italingana na namba ya swali lake lililoko juu.

1. Ni rahisi zaidi kuanzisha kanisa mahali ambapo watu wengi huishi. Ni vigumu kuanzisha kanisa ambapo watu ni wachache na wanakaa mbalimbali kwa sababu washiriki watakuwa wachache.

2. Ni vigumu kuanzisha kanisa ambapo lugha ni nyingi na watu hawasemi lugha moja tu. Kwa hiyo, lazima ujue wanapendelea lugha gani zaidi, ili uweze kutafuta wafanya kazi wanaoweza kusema kwa lugha ile na kutayarisha vifaa katika lugha ile.

3. Ikiwa watu wengine wanahamia mahali pale, labda kanisa litakua vizuri. Kwa upande mwingine, ikiwa watu wanahama, pengine siku moja kanisa jipya lile litakuwa halina washiriki.

4. Yakiwa makanisa machache, au hamna makanisa kamwe, watu watafurahi kanisa lianzishwe. Walakini yakiwepo makanisa mengi, watu hawatafurahi ukilianzisha lingine. Watadhani labda utawavuta baadhi ya washiriki wao.

5. Kulingana na namba tatu, barabara, shule, na maduka huonyesha maendeleo. Mahali ambapo vitu hivi havipo, wakati ujao hauwezi kuhesabiwa kuwa mzuri. Pengine, kanisa jipya halingeweza kukua. Pia, mara nyingine, ni

vizuri kujenga kanisa ambapo kuna shughuli nyingi na watu waweza kuliona na kujua habari yake.
yake.

6. Ukiweza kuwasaidia watu na mahitaji yao, itakuwa rahisi zaidi kuanzisha kanisa. Watu watafurahi na kuwepo tayari kuisikiliza mahubiri yako baada ya kusaidiwa nawe.

7. Kila mahali kuna watu kadha ambao hukata mashauri kama viongozi; kisha, watu wengi wengine huufuata uamuzi wao. Ikiwa mmojawapo wa hawa wenye kukata mashauri atapatwa kuwa Mkristo na kulihudhuria kanisa lako, wengi zaidi watamfuata na kuja pia. Na yawezekana hawa wataamini pia.

8 na 9. Si rahisi watu wavutwe na mtu ambaye ni mgeni. Lakini, ikiwa rafiki zao za Kikristo au jamaa zao wanaishi katika mahali fulani na wamejulikana, watu waishio pale watawasikiliza. Watu huweza kuvutwa rahisi zaidi kwa neno la wenzao ambao wanawafahamu na kuwaheshimu.

10. Mara nyingi, watu wa mahali fulani wataamini upesi ujumbe maalum wakiwa wanakataa ujumbe mwingine wa kawaida. Ujumbe utakuwa "maalum" kwao kwa sababu ya imani, mila, au mahitaji yao. Kwa mfano, pengine wanayo imani fulani ya kienyeji juu ya dhabihu ya damu inayoweza kuwasaidia waelewe juu ya kifo cha Yesu. Au pengine wamekuwa na shida katika kijiji chao inayoweza kusaidiwa na mafundisho ya Biblia. Uombe kwamba Mungu atakusaidia kutambua ile njia ya kuwavutia.

11. Ni muhimu kukutanika katika mahali pale pale kila Jumapili. Mahali pakibadilishwa, wengine watachanganyikiwa. Pangekuwa mahali pazuri, pa kupendeza, bila usumbufu ili watu wafurahi na kutokatishwa tamaa wasirudi tena.

12. Bila shaka ushirika wa wakuu wa kijiji na serikali ni kitu cha kutafutwa. Kwa mfano, ikiwepo sheria inayokataza mikutano isiwepo saa za usiku, sheria hiyo ingetiiwa. Maana, sehemu mojawapo ya kazi ya kanisa ni kujenga hali uzuri wa kijiji na taifa.

Baada ya kuchunguza maeneo mawili au matatu, uyalete matokeo ya uchunguzi huo mbele ya wazee au mashemasi wa kanisa lako. Toa taarifa kamili juu ya majibu uliyoyapata kwa yale maswali kumi na mawili. Mwongeane juu ya yale ambayo Mungu anawaonyesha katika majibu hayo. Kisha, pamoja, nyinyi mwamue: Je, Mungu anataka tulianzishe kanisa katika eneo moja kati ya hayo mawili au matatu ama sivyo?

## *HATUA 4: TEMBELEA JAMAA.*

Katika Matendo 16:34-35 tunasoma juu ya ushuhuda wa Paulo kwa jamaa moja. Aliiambia jamaa nzima Neno la Mungu. Yesu pia, alitumia njia hiyo ya kutembelea jamaa. Zifuatazo ni jamaa kadhaa alizozitembelea Yesu:

1. Jamaa ya Simoni Petro (Marko 1:29-31).
2. Jamaa ya Mathayo (Mathayo 9:9-13).
3. Jamaa ya Mariamu, Martha na Lazaro (Luka 10:38-42).
4. Jamaa ya Farisayo (Luka 11:37).

Yesu hupenda kazi yako ifanane na kazi yake. "Kama baba alivyonituma mimi, mimi nami nawapeleka ninyi" (Yohana 20:21). Yeye ni kielelezo chetu hata katika kazi yetu. Katika Yohana 15:16, Yesu anatuambia "Mwende mkazae matunda." Ukiwa unatembelea jamaa nyumbani za watu, utazaa

matunda. Katika nyumba za watu unaweza kufundisha Biblia kwa jamaa nzima. Wewe na wasaidizi wako mnaweza kutembelea jamaa mkisikiliza mahitaji na shida zao. Mnaweza kuwashuhudia juu ya uwezo wa Kristo kuokoa na mtawasaidia watu kumpokea Kristo kama Mwokozi.

Katika Matendo 20:20 twasoma kuwa Paulo alifundisha watu akienda nyumba kwa nyumba. Wewe pia na wasaidizi wako mngeenda nyumba kwa nyumba. Hii ni muhimu sana. Katika nyumba mtawatembelea wanawake na wanaume ambao wamepotea. Mtakapofika kwenye nyumba, omba kuzungumza na mwanaume anayeishi hapo. Zungumza na wazee kwani wanasikilizwa na jamaa nzima. Ijapokuwa wanaume hao watakuwa hawaitikii Habari Njema upesi, onyesha heshima kwa kuzungumza nao kwanza. Vijana pia wanatakiwa kuvutwa kwa Yesu.

Naam, wanawake pia ni watu maalum. Mungu awapenda wanawake sana na wameimarisha makanisa mengi kwa kazi zao. Hivyo, unapotembelea jamaa, waambie wanawake juu ya Yesu na kanisa lake. Shabaha yako ni lazima iwe kuwavuta wanawake na wanaume wapotevu. Wapotevu hawa ambao hawajampokea Kristo ndio wasioamini. Wapotevu ni watu ambao ni lazima wazaliwe mara ya pili. Wewe na wasaidizi wako mtawashirikisha hawa wapotevu Habari Njema. Lengo lako katika kuanzisha makanisa mapya liwe kuwaleta wanaume, wanawake, na vijana kwa Yesu Kristo.

Usiibe kondoo! Hii inamaanisha usijaribu kuwavuta washiriki kutoka kwenye makanisa mengine. Tunajenga ufalme wa Mungu tunapowavuta wapotevu kwa Yesu. Utaisikia furaha ile ile aliyoisikia baba na mwana mpotevu utakapowavuta wapotevu: "Mwanangu alikuwa amekufa, naye amefufuka; alikuwa amepotea, naye ameonekana". Washiriki "baridi" kadhaa wanaweza kufufuliwa kiroho na kujiunga na kanisa jipya, lakini ni vema zaidi kuwatembelea wapotevu.

Inawabidi pia kuwatembelea ndugu na marafiki wa washiriki wenu. Unaweza kupeleleza zaidi juu ya watu hawa kanisani kwako. Washiriki wanaweza kuandika majina na anwani za ndugu au marafiki zao wanaoishi katika eneo ambapo mnaazisha kanisa. Jinsi Andrea alivyomleta ndugu yake Petro kwa Yesu (Yohana 1:40-42), hivyo ndivyo washiriki wa kanisa lako wanavyohitaji kutamani kuwaleta ndugu zao kwa Yesu. Kama Kornelio alivyowaita ndugu zake na marafiki wake wakuu (Matendo 10:24), vile vile washiriki wa kanisa lako wanaweza kukusaidia kuwatembelea ndugu na marafiki zao.

Wakati utakapotembelea jamaa, utazungumzia nini? Zungumza juu ya Yesu, Biblia na kanisa. Zungumza zaidi juu ya **Yesu;** yeye ndiye kiini cha ujumbe wetu. Waambie watu juu ya nguvu na upendo wa Yesu Kristo. Eleza habari za maajabu na miujiza alivyovifanya Yesu. Ule ujumbe wa mitume ulikuwa Habari Njema ya Yesu. Walizungumza kuhusu kifo (Matendo 2:22-23) na ufufuo wa Yesu (Matendo 4:33).

Zungumza pia juu ya **Biblia,** kwani Mungu huweza kufundisha watu mambo mengi wakiwa wakijua Biblia. Nenda na Biblia yako wakati wa kutembelea jamaa. Soma kutoka kwa Neno la Mungu, ukiwaonyesha kwamba Biblia inayo majawabu ya matatizo yao. Shirikisha Neno kwa moyo mjasiri (Matendo 4:31).

**Kwa hiyo ukiwa** unakwenda nyumba kwa nyumba, zungumza juu ya **Yesu,** **Biblia,** na **kanisa.** Waeleze wote jinsi kanisa lako limesaidia kijiji au mji wako. Zungumza juu ya ulazima wa watu kuwa na makanisa karibu na nyumba zao. Kwani makanisa yanaweza kuwasaidia watoto wao na kubadilisha maisha ya wote watakaoamini. Vifuatavyo ni vifungu vichache vinavyohusiana na kanisa: MATHAYO 16:18, MATENDO 11:26, na WAEFESO 5:23-25. Waarifu wale unaowatembelea ya kuwa unataka kuwasaidia kuanzisha kanisa jipya. Waambie ya kuwa Mungu anapenda wajue zaidi juu ya Yesu, Biblia, na kanisa.

Mwisho, utakapokuwa ukitembelea jamaa zile, hakikisha:

A. Uwasikilize watu.
B. Uwasaidie watu.

Sikiliza kwa makini watu ambao unawatembelea nyumbani kwao. Jaribu kuelewa jinsi wasikiavyo moyoni. Yaani, Je, wamechoka? Wana njaa? Wanasikia upweke au hofu? Je, wanafikiri kwamba mtu fulani amewalaani? Kuna aliye mgonjwa? Watu wanahitaji nini hasa? Shida zao ni zipi? Je, wana shida za ndoa au kuzinaa? Je, wanazo shida za watoto au hawana kazi? Hivyo sikiliza sana watu hawa wazungumzapo juu ya shida na mahitaji yao.

Jaribu kuwasaidia watu. Mara nyingine jambo hili ni gumu. Lakini kama unapenda watu, utajaribu kuwasaidia. Zifuatazo ni njia tano za kusaidia watu:

1. Unaweza kusaidia kwa kuwasikiliza.
2. Unaweza kuwasaidia kwa kuwadokezea majawabu kwa shida zao.
3. Unaweza kusaidia jamaa kwa kuwasomea Biblia na kuomba pamoja nao.
4. Pengine unao washiriki wa kanisa lako wanaoweza kufika na kusaidia.
5. Unawasaidia unapowaambia watu juu ya Yesu, Biblia na kanisa.

Kwa hiyo, nenda kutembelea jamaa. Uwasikilize na uwasaidie. Hakikisha unajaribu kuvuta jamaa nzima kwa Kristo. Uwaeleze watu juu ya kuokolewa kwako na maisha yako ya Kikristo. Viachie Biblia na Roho Mtakatifu kufanya kazi yao. Tumia vifungu kama hizi: Yohana 3:16, Warumi 3:23, Warumi 6:23, Yohana 1:23 na Matendo 16:32. Mungu awabariki wewe na wasaidizi wako mkiwavuta watu kwa Kristo: Bwana awapeni nguvu mkitembelea jamaa!

## HATUA 5: TAFUTA MAHALI PA KUKUTANIKA.

Wakati mnapotembelea jamaa, labda watu watauliza: "Kanisa jipya litakutana wapi?" Ni wazi haiwezekani kuwa na kanisa kama hakuna mikutano ya kuabudu na kushirikiana na kufundisha. Kwa hiyo, ni lazima patafutwe mahali ambapo waamini wa Kikristo wanaweza kukutana na kuomba, kujifunza na kushirikiana.

Zifuatazo ni mahali sita ambapo kanisa jipya linaweza kuanzisha mikutano:

1. Katika nyumba ya mtu.
2. Katika shule.
3. Chini ya mti.
4. Dukani.
5. Katika jumba la mji.
6. Katika jengo dogo ambalo mnaweza kujenga kwa gharama ndogo.

Vifungu kama I Wakorintho 16:19, Wakolosai 4:15 na Filemoni 1:2 vinaonyesha kwamba makanisa yanaweza kukutana kwenye nyumba. I Wakorintho 16:19: "Akila na Prisila wawasalimu sana katika Bwana, pamoja na kanisa lililoko ndani ya nyumba yao."

Mfano wa kanisa lililokutanika katika nyumba ni kanisa moja jipya humo Nairobi, Kenya, lililokutana kwa miezi mingi katika nyumba ya Daudi na Priscila Masika. Walitoa Agano Jipya na vitabu vya nyimbo vichache. Daudi alizungumza na marafiki zake kazini, na Priscila aliwashuhudia wanawake na vijana waliopotea. Hivyo watu walikaribishwa nyumbani ya Masika kuimba, kuomba na kujifunza Biblia.

Kanisa lililoko Kalulu, Kenya, lilianzishwa chini ya mbuyu. Kilichofanyika ni kwamba kichaka kilichokuwa chini ya mbuyu ule kilifyekwa. Viti vichache vilitengenezwa kutoka kwa magogo. Jamaa walitembelewa na kukaribishwa kwenye ibada. Sasa kanisa hilo linalo jengo. Lakini kwa muda wa karibu mwaka moja, walikutana chini ya mbuyu.

Kanisa la Kibatisti la Il Mamen ni kanisa jipya kati ya Wamaasai. Waamini hao wapya hukutana katika jengo la shule ya msingi ya Il Mamen kila Jumapili. Wamaasai wengi, wanaume kwa wanawake kwa vijana, huja shule hiyo kuabudu. Shule inajulikana sana na ipo katikati ya watu. Kuna ubao ambao mchungaji huutumia akifundisha Biblia.


Zaidi ya mwaka mmoja mikutano ya Kikristo iliendeshwa kwenye jengo la umma la Jeriko katika Nairobi, Kenya. Kikundi cha watu kilivutwa kwa Kristo. Waamini hao walisali na kujifunza kwenye jengo hilo. Sasa kuna kanisa la Kibatisti kule Jeriko.

Huko Ngwate, Kenya, ndugu wawili waliopenda watu walitembelea nyumba kwa nyumba. Mkazo wao wa kwanza ulikuwa kazi ya kuwavuta watu kwa Kristo. Mara jengo lilihitajika kwa ajili ya Shule ya Jumapili na ibada. Kwa vile Ngwate ni kijiji kilicho mashambani ardhi ilikuwa si ghali. Viongozi waliweza kupata kiwanja kilichokuwa karibu na shule. Fedha zilichangwa na jengo la kanisa likajengwa. Kutokana na kanisa hilo la Ngwate, makanisa mengine matano yameanzishwa kwa mtindo huo huo mnamo miaka miwili iliyopita.

Hivyo, mikutano ya kanisa jipya linaweza kuanzishwa kwenye nyumba, au shule, chini ya mti, dukani, au kwenye jengo lolote la umma, hata kwenye nyumba ndogo iliyojengwa na kanisa isiyogharimu fedha nyingi. Kila mahali mikutano itakapofanyika ni muhimu kuchagua mahali ambapo ni katikati ya watu, kama shule, karibu na barabara au mahali penye maduka. Ni lazima pawe mahali ambapo watu wanaweza kupafikia kwa haraka zaidi na bila ugumu wowote.

Tayarisha mikutano kwa kusafisha mahali pa mkutano - nyumba au chini ya mti. Mungu hupendelea mahali pa kumwabudia pawe safi. Watu hawapendi kuhudhuria kwenye kanisa chafu lisilovutia. Kwa mfano, hivyo ndivyo mahali pamoja fulani palivyotayarishwa: Mchungaji wa kundi jipya la Masalani aliwaomba Wakristo wapya kufyeka majani yaliyokuwepo chini ya mti mkubwa. Kisha viti sita vilitengenezwa na msalaba mdogo ulitundikwa kwenye mti. Watu hawa walifanya mahali pale safi, penye kuwa tayari kwa ibada. Leo kanisa hilo la Masalani limekua kuwa imara ya kutosha lisaidie kuyaanzisha makanisa mawili mapya mengine.

Sasa, kwa kifupi tuzichunguze hatua hizi tano tena. Zifuatazo ni hatua tano juu ya kuanzisha kwa makanisa mapya:




Hakikisha unafanya kila kitu unachojifunza katika kitabu hiki. Ni vibaya sana kushindwa kutekeleza wito wa Mungu. Mungu hupenda makanisa yakue na kuzaa makanisa mengine. Anataka kukuona ukiwavuta wapotevu na kuyaanzisha makanisa mapya. Zidi kuomba unaposoma kitabu hiki.

Mwombe Mungu akuongoze hatua kwa hatua uendapo ukitekeleza yale unayojifunza kutoka kwa kitabu hiki.

Sasa tujifunze hatua ya sita na ya saba. Hatua hizi mbili za mwisho za kuanzisha makanisa ni muhimu sana. Kama unatenda kwa uaminifu yaliyosemwa katika hatua moja hadi tano, sasa uko tayari kwa hatua ya sita.


## *HATUA 6: ANZISHA MIKUTANO*

Mikutano ya Kikristo kwa kuabudu, kutiwa moyo, na kushirikiana ni kitu kilicho kiini cha maisha ya kiroho. Kuabudu kwa kweli huwaandaa waamini kwa kazi ya Kristo siku kwa siku. Yesu alisema katika Yohana 4:23, "Waabuduo halisi watamwabudu Baba katika Roho na kweli. Kwa maana Baba awatafuta watu kama hao wamwabudu."

Mwandishi wa kitabu cha Waebrania ni wa msaada kwetu, akielezea juu ya tabia ya mikutano ya Wakristo. Katika Waebrania 10:25, tunaambiwa: "Wala tusiache kukusanyika pamoja." Vifungu vingine katika Waebrania 10 vyatuonyesha kielelezo cha yale yanayopaswa kuonekana katika mikutano ya Kikristo: "na tukaribie wenye moyo wa kweli kwa utimilifu wa imani" (kifungu 22); "Tukaangaliane sisi kwa sisi na kuhimizana katika upendo na kazi nzuri" (kifungu 24); "tuonyane" (kifungu 25).

Kusudi la mikutano ya Kikristo ni kujenga imani ya waamini na kuwavuta wasio Wakristo kwake Kristo, wampokee ili awe Bwana na Mwokozi wao. Hapo zamani, katika makanisa machanga aliyoanzisha Paulo, ibada ziliwaweka binadamu karibu na Mungu. Ilikuwa si lazima mtu aitishe ibada; bali waamini walitembeleana na kukutana, "wakifundishana na kuonyana" kwa hekima yote (Wakolosai 3:16). Wakristo waliambiwa, "msemezane kwa zaburi [illegible] na nyimbo za

rohoni, huku mkiimba na kumshangilia Bwana mioyoni mwenu" (Waefeso 5:19). Kwa hivyo, unapoanzisha ibada za kanisa jipya, fuata maagizo ambayo Mungu aliwapa Wakristo hawa wa kwanza.



Moja ya mikutano mizuri kwa kanisa jipya ni **mkutano wa kusoma na kujifunza Biblia.** Anaweza kutafutwa mtu fulani ambaye anaweza kusoma vizuri Neno la Mungu. Inafaa kutumia lugha inayotumika na watu wa eneo hilo kwa kujifunzia Biblia. Kutafakari vifungu na mazungumzo kunaweza kusaidia pia. Lakini mkazo mkuu ungekuwa kumpa Roho Mtakatifu nafasi azungumze na kila mmoja waziwazi kwa njia ya kusoma Biblia kwa uangalifu. Maandiko kutoka kwa Biblia yachaguliwe mapema, tena yalingane na mahitaji ya

kiroho ya watu, na upelekaji wa Injili kwa njia ya kusoma Biblia. Inambidi msomaji ajitayarishe kusoma Neno la Mungu mbele ya watu; atafanya hivyo kwa kujizoeza kusoma mapema, tena kwa sauti, maandiko aliyochagua.

Mikutano ya kusoma na kujifunza Biblia imeanza kutumika kuwavuta waamini wapya na kuanzisha makanisa mapya huko Bangladesh. Maelezo ya mpango huu, ambao Mungu ameubariki na kuutumia kuwavuta Waislamu kwa Kristo, yataletwa baadaye katika kitabu hiki.

Mikutano ya kusoma Biblia ilianzishwa hivyo huko Guatemala: jamaa zilitembelewa, na watu kadhaa wakavutwa kwake Yesu. Kisha ibada zilianzishwa kwenye nyumba, shule, na majengo mengine. Injili ya Yohana ilichaguliwa kusomwa kutoka kwenye Biblia. Mungu aliutumia usomaji huo na kutafakari kifungu kimoja cha Neno lake kuanzishia makanisa mapya huko Guatemala.

Pengine utapenda kuwa na madarasa ya kusoma Biblia kama njia nzuri ya kuanzishia makanisa. Ukitaka kusoma Injili ya Yohana, tumia vifungu hivi:

1. Yohana 1:6-9, 19-34 ___ Yohana Mbatizaji.
2. Yohana 4:4-29, 39-42 ___ Mwanamke Msamaria.
3. Yohana 20:1-10, 19-31 ___ Mitume wasioamini.
4. Yohana 3:1-18 ___ Nikodemo.

Twasoma katika Matendo ya Mitume 2:42, "Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika." Watu hurudi kwenye ibada tena na tena wanapokuta "ushirika na fundisho" yenye nguvu. Kanisa jipya linaweza kufurahia kukua kwake kama vile kanisa la Beroya lilivyofurahia: "Walilipokea lile neno kwa uelekevu wa moyo, wakayachunguza maandiko kila siku, wengi wao wakaamini" (Matendo 17:11-12). Ni furaha ya ajabu kuona watu wakisoma Neno la Mungu pamoja! Ni furaha ya ajabu kuona "Kitabu cha Mungu" kikitoa majibu ya Mungu kwa watu wa Mungu!

Kama mnayo mikutano ya kusoma Biblia, yafuatayo ni mapendekezo machache:

1. Uwe mwalimu mwenye furaha. Furahia darasa la kujisomea Biblia.
2. Weka mambo yote kuwa ya kawaida na ukaribishe majadiliano.
3. Linganisha somo na hali halisi ya maisha.
4. Uwe kirafiki, na mwenye kupenda kusikiliza mahitaji ya wote.
5. Sema ukweli katika upendo.
6. Jifunze sura moja ya Biblia badala ya kutafuta vifungu vingi mbalimbali.
7. Karibisha maswali.
8. Tembelea jamaa kuhakikisha kuwa wasio Wakristo wanahudhuria mikutano ya kujifunza Biblia pia.
9. Anza kwenye mkutano wa kwanza kuchunguza anayeweza kuwa kiongozi wa darasa hilo baadaye.
10. Kusudia kuwavuta watu kumpokea Kristo na kukua katika imani.

Soma tena orodha hii ya mapendekezo. Uyafuate kwa makini. Ukiliongoza darasa, yarudie mapendekezo haya mara kwa mara.

Katika kuanzisha makanisa mapya, mkutano mwingine wa Kikristo ni: Mikutano ya kuabudu. Soma Zaburi 95:1-6 na 100:1-5 kujifunza zaidi juu ya ibada. Kanisa lililopo Utu, Kenya, lilianzishwa na mikutano ya kuabudu. Ndugu Paul Mung'au na wanaume wawili wengine walitembelea jamaa hapo Utu. Walitangaza Habari Njema ya Kristo, kisha watu walianza kumpokea Kristo kuwa Mwokozi wao. Mahali pa kukutanika palikuwa chini ya mti mkubwa, karibu na shule. Ndugu Mung'au aliwakaribisha watu wengi, waje kumwabudu Mungu wa kweli aliye hai. Watu wakaja na kanisa la Utu lilianzishwa kwa njia ya kuwa na mikutano ya kuabudu. Njaa na kiu ya kumjua Mungu, hamu ya watu kuimba, kuomba, na kumsifu Mungu, vyote vilisaidia uanzishaji wa kanisa la Utu. Utamu wa kumjua Mungu mwenyewe ulizaa kanisa jipya!

Mikutano ya kuabudu yanakata kiu chetu cha Mungu. Hakikisha kuwa unaanzisha kanisa jipya kwa kuwa na ibada zinazoleta utukufu kwa Mungu. Watu wanapozidi kujishirikisha, uwasaidie wamtambue Mungu ya kuwa yeye ni Mungu. Wajue Mungu ndiye chanzo cha nguvu na raha. Wakati Mungu akiwepo katika ibada kweli kweli, maisha hubadilishwa, dhambi husamehewa na imani huwa na nguvu zaidi.

Ibada iwe katika lugha ambayo watu wa eneo hilo wanatumia nyumbani. Kwa kifupi, ufuatao ni mpango wa ibada katika kanisa jipya.

Soma Zaburi fupi.
Imbeni wimbo mmoja au mbili.
Soma maandiko kutoka Biblia yanayolingana na mahubiri.
Imbeni wimbo mwingine.
Pokea matoleo na sadaka.
Wimbo maalum na waimbaji (au wote kwa jumla).
Mahubiri yanayofundisha na kuonyesha jinsi Neno la Mungu linavyohusiana na maisha ya watu.
Mwaliko wa kumpokea Kristo.
Wimbo wa mwisho na maombi.
Toa matangazo kwa kifupi.

Mpango huo unaweza kubadilishwa ikiwa Mungu anakuongoza. Kwa mfano, pengine utapenda kuwa na wakati wa maombi ya pekee kimya kimya, au wakati wa ushuhuda.

Katika mikutano ya kanisa jipya, mtegemee Roho Mtakatifu. Roho wa Mungu huleta nguvu katika mikutano ya Kikristo. Katika ushirika wa Kikristo hatuna budi kuishi na kutembea katika Roho. Katika mikutano yenu, Roho Mtakatifu ataleta upendo kati yenu (I Yohana 4:11-13). Na Roho wa Mungu atakuelewesha lile Neno (Yohana 14:26). Ni ombi langu kuwa, utakapoanzisha mikutano ya kanisa jipya, Roho Mtakatifu atakufundisha, atakutuliza, atakuongoza na kukupa nguvu.

## HATUA 7: MTAFUTE NA KUMFUNDISHA KIONGOZI

Unahitaji kiongozi anayefaa katika kanisa unaloliaanzisha. Maana itakubidi wewe urudie kwenye kanisa lako. Pia, labda utapenda kwenda sehemu nyingine kuanzisha makanisa mapya.

Kwa hivyo, ni lazima umtafute na kumfundisha kiongozi atakayeendelea na kazi ya kanisa hilo jipya. Anatakiwa kuwa kiongozi anayeweza kuwa "Mchungaji wa kundi la Mungu", tena mwenye kuweza kuliongoza kanisa hilo changa kukomaa. Kanisa jipya litakua ama kuanguka kufuatana na uongozi wake. Mtafute mchungaji anayeweza kukua katika wakati wa Mungu kuwa mtu wa Mungu katika kanisa la Mungu.

Utambue, si kazi yako peke yako kumtafuta kiongozi. Hilo ndilo jambo ambalo utalifanya pamoja na Mungu na pamoja na washiriki wa kanisa hilo jipya. Tunastahili kutoa shukrani nyingi ajabu kwamba ni Mungu anayewaita viongozi, si sisi! Ni wajibu wa Mungu kumpata atakaye kuwa kiongozi cha watu wake. Katika kazi hii ya kumtafuta mchungaji na kumfunza kazi, unaweza kumtegemea Mungu kwa nguvu yako na kukuongoza. Washiriki wakiwa wanamchagua kiongozi wao, uwashauri wamtegemee Mungu.

Yafuatayo ni mambo kadhaa ya kufuata wakati mtakapokuwa mkimtafuta mchungaji wa kanisa jipya.

KIONGOZI ANAYEFAA HUPASWA:

1. Awe mwaminifu kwa Kristo.
2. Awe tayari kujifunza.
3. Awe ameitwa na Mungu.

"Kuwa mwaminifu kwa Kristo" inamaanisha, kwanza kabisa, kiongozi ni lazima awe amezaliwa mara ya pili. Yaani, awe mtu aliyetubu dhambi zake na kumpokea Kristo kama Mwokozi wake. Uwe mwangalifu sana katika jambo hilo. Wasaidie washiriki wa kanisa hilo jipya kumtafuta mchungaji ambaye ameokolewa kweli, na amejitoa hasa kwa Mungu. Paulo alimwambia Timotheo kuchagua watu waaminifu (II Timotheo 2:1-2). Mchungaji ni lazima awe mtu anayejiweka mbele ya Mungu kila siku, akitoa maisha yake, mapenzi yake na uwezo wake kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.

Pia, kuwa tayari kujifunza ni muhimu sana kwa wachungaji wapya. Yawezekana mtu ambaye Mungu anamsimamisha kuwa kiongozi hatakuwa na uwezo mkubwa sana. Katika I Wakorintho 1:26-29 Paulo anasema kwamba si wengi wenye nguvu au utajiri wanaoitwa na Mungu. Mara nyingine Mungu huchagua hata waliodhaifu kuwa wachungaji! Lakini hamu ya Mungu ni kumjenga huyu kiongozi dhaifu mpaka atakapokuwa na nguvu. Hivyo tafuta mtu ambaye yuko tayari kujifunza. Tafuta atakayejifunza kutoka kwa Biblia na kutoka kwako. Kama mchungaji mpya anapenda Neno la Mungu, utaweza kumfunza.

Hakuna mchungaji anayeweza kufaulu katika kazi yake bila wito wa Mungu. Kwa njia ya kusoma Neno la Mungu na kwa kuelewa kunakotolewa na Roho Mtakatifu, Mungu hudhihirisha wito wake wazi. Wito wa uchungaji ni maalum na wa pekee. Unaweza kumsaidia mchungaji mpya aelewe wito wa Mungu kwa kujifunza pamoja vifungu vifuatavyo:

1. Kuitwa kuwa mtumishi, Mathayo 23:8-12 na Luka 22:26-27.
2. Kuitwa katika huduma ya lile Neno, Waefeso 4:11-16 na I Petro 4:7-11.
3. Kuitwa kuwa shahidi wa Kristo, Matendo 1:21-22 na Matendo 10:39-43.
4. Wito kwa kazi maalum, Timotheo 3:1-7.
5. Kuitwa kuwa mchungaji, I Petro 5:1-4.

Labda unafikiri kumpata mchungaji ambaye ni mwaminifu na mwenye wito ni vigumu. Ni kweli! Haitakuwa rahisi kumpata mtu ambaye Mungu anataka awe mchungaji wa kondoo zake. Lakini kwa kuwa twajua kwamba hakuna lisilowezekana kwa Mungu, tungejua pia ya kuwa "utoshelevu wetu watoka kwa Mungu" (II Wakorintho 3:5). Mungu atakupa busara na uongozi wote katika kutoa mashauri juu ya mchungaji mpya.

Ni muhimu kukumbuka kwamba, kawaida si busara kuleta mchungaji kutoka nje ya mahali kanisa lilipo. Ni bora kwa kanisa jipya kuwa na **kiongozi anayeishi na watu wake.** Angekuwa mtu azungumzaye lugha yao na kuelewa shida zao.

Mungu akiwa anamwita na kumsimamisha mchungaji kwa ajili ya kanisa jipya, mfundishe kiongozi huyo kweli hizi:

1. Ni lazima amtegemee Mungu, Wafilipi 2:13, na II Wakorintho 12:9-10.
2. Afanye kazi kwa ubora, Marko 12:29-30; Warumi 12:11; II Timotheo 3:16-17.
3. Ni lazima awasaidie washiriki kirohoni, Mathayo 5:1-2 na I Wathesalonike 2:11-12.

Msaidie kiongozi "kujilisha". Hivyo ni kusema, mwonyeshe kiongozi huyo namna ya kujilisha mwenyewe kirohoni kwa kusoma Biblia kila siku, kwa kuomba, na kwa kusoma vitabu maalum kwa wachungaji. Mfundishe mchungaji kusoma Biblia, kutafakari na kukariri Neno Takatifu la Mungu. Dhihirisha umuhimu wa maombi kwa njia ya kuomba naye kila mara. Msaidie kiongozi huyo kuweza kuwa na "wakati wa kimya" kila siku wa maombi, akiwa na orodha wa mambo ya kuyaombea na Biblia ambayo imefunguliwa wazi. Ikiwezekana, mwambie kiongozi huyo kujiunga na darasa la kujisomesha kithelogia nje ya shule (yaani: "Theological Education by Extension" TEE), au Shule ya Biblia, au somo la

Biblia kwa njia ya posta. Angeanza mapema kabisa kusoma vitabu vya TEE kama **Mchungaji na Kazi Yake**, na **Kuleta Watu kwa Kristo.**

Wakati fulani baadaye, pengine itakuwa busara kuzungumza na mchungaji na waamini juu ya kuunda kanisa. Yawezekana makanisa au madhehebu fulani hayatapendelea kuunda kanisa kirasmi kama chama, hasa vijijini. Pengine hudhaniwa kutokuwa muhimu katika kukua kwa kanisa yanayozaliana haraka.


Lakini, sheria ya kiserikali katika nchi nyingine zalazimisha kwamba kanisa liundwe kirasmi na kuandikishwa kabla ya kuwa na ruhusa kutoza pesa katika sadaka. Pia, kama kanisa lako ni mshirika wa dhehebu fulani, yawezekana dhehebu lile limekwisha kuwa na katiba itawalayo makanisa yake yote. Yawezekana limeandikishwa na serikali kama kanisa (dhehebu), chama cha ushirika, au chama kuwasaidia watu.

Ikiwa kanisa lako si katika dhehebu, unaweza kuchagua kamati ya kutayarisha katiba iliyo rahisi. Kamati hiyo ingefanya kazi pamoja na wazee au mashemasi ya kanisa lililoanzisha na kusimamia kanisa lako. Katiba ikiwa imekubaliwa na kura za washiriki wake, kanisa linaweza kutambulika kwamba limeundwa kirasmi.


Makanisa mapya yote yatahitaji uelewano, ambao una msimamo wa Kibiblia kuhusu maswali kama hayo: Imani zetu kubwa ni nini? Viongozi wa kanisa letu watakuwa nani? Kazi zao ni nini? Tutapataje gharama ya shughuli za kanisa letu? Tutashirikishwa na nani? Mara nyingi maswali hayo yanajibiwa katika katiba iandikwayo na sheria zake.

Sasa tumekwisha chunguza zile hatua saba zinazoeleza jinsi ya kuanzisha makanisa mapya.

Angalia tena hatua hizi za Mpango Maalum wa Kimsingi:




Yesu alisema, "mavuno ni mengi" (Mathayo 9:37). Na neno lake litutie nguvu na kutuwezesha kufanya vitendo vya ujasiri! Tunao ujumbe mkuu wa kutangaza! Ujumbe huu unahusu HABARI NJEMA za wokovu wa Mungu kwa njia ya Kristo. Ni habari ya upendo na ukombozi wa Mungu kwa ulimwengu. Kazi yetu kubwa ni - kuwaeleza wengine juu ya Yesu na kuanzisha makanisa, ambayo yataendelea kuwaambia wengine juu ya Yesu. Mungu akubariki utakapozidi kuwavuta watu kwa Kristo na kuwaongoza kufanya kazi yake na kumwabudu pamoja, wakiwa kama kanisa jipya.




# II

# MIPANGO MINGINE KWA KUANZISHA MAKANISA

Mipango ifuatayo imetolewa ili kuwa nyongeza juu ya namna ya kuanzisha makanisa. Wako watu katika maumbile mbalimbali; vazi moja haliwezi kuwatosha wote. Vivyo hivyo, kuna mazingira mbalimbali. Pia, kuna shida zinazohusika kuanzisha kwa makanisa. Kwa hiyo tunalazimishwa tuwe na mitindo ya mipango mingi. Hivyo, unaombwa kusoma mawazo hayo. Uombe, ukiyatafuta mawazo mapya ambayo pengine Mungu atayatumia katika hali yako.

Katika uanzishaji wa makanisa kuna vipindi mbalimbali vya ukuzi. Vipindi hivyo vinaweza kuchorwa kama ifuatavyo:

# VIPINDI VYA UKUZI WA KANISA



Vipindi hivi vya kukua hadi kuwa kanisa kamili vina mwanzo wake katika **kipindi cha 1:** "Watu wasikia Injili." Zile mbegu za Injili hupandwa na wale wanaokwenda ulimwenguni wakishirikisha ile Habari Njema. Watawasababisha watu watambue wokovu uko katika Kristo. Katika **kipindi cha 2:** Kuna ongezeko la ujuzi wa ukweli wa Habari Njema, kindani zaidi. Hasa ni ujuzi juu ya dhambi za binadamu na upekee wa Yesu Kristo. Roho Mtakatifu huutumia ujuzi huo kuleta hamu ya mabadiliko katika maisha ya watu.

Katika **kipindi cha 3:** Watu hukata shauri kujitoa kwa Kristo. Mbegu za Habari Njema zimekua katika udongo mzuri. "Aliyelisikia neno hulielewa" - Mathayo 13:23. Katika **kipindi cha 4:** Ndipo uamuzi wa kubadilisha maisha hufanywa kwa kutubu na kuamini katika Kristo (Marko 1:15).

**Kipindi cha 5:** Hawa ambao wameamini waunganwa katika kundi linaloitwa "KANISA". Kundi laweza kuitwa "kanisa" wakati ambapo kundi la watu ambao wametubu dhambi zao na kumwamini Kristo wataungana katika ushirika wa mwili wa Kristo. Ndipo watu hawa wapya katika Kristo (II Wakorintho 5:17) huanza kukua kirohoni. Watakua kwa kujua Biblia, katika **kipindi cha 6;** na kwa ibada na ushuhuda katika **kipindi cha 7.** Mwisho, vipindi hivyo huanza kujirudia vyenyewe, jinsi kanisa linavyoanzisha kanisa lingine, **kipindi cha 8** (Mathayo 28:20 na II Timotheo 2:2). Makanisa mapya "yatapandwa" jinsi "ardhi" nzuri inavyozidi kugunduliwa.

# A. MPANGO WA KUTUMIA VIKUNDI

Kwa kutumia mpango wa vikundi (yaani timu), kwenye eneo la pwani ya Afrika ya Mashariki, zaidi ya makanisa 50

yalianzishwa. Ushindi huu kwa ajili ya Kristo ulikuja wakati watu zaidi ya 3,000 walikuwa wakiokolewa na Yesu, na kubatizwa. Kazi ya uinjilisti na mwagiko wa baraka za Mungu vinatukumbusha siku ya Pentekoste! "Walilipokea neno...wakabatizwa...wakajiweka wakfu katika mafundisho na ushirika...maombi...na kumsifu Mungu" (Matendo 2:41-47). Hivi ndivyo Mpango wa Kutumia Vikundi unavyofanya kazi:

### 1. Chagua na Kuvitayarisha Vikundi

Omba Mungu awaite watu wanne, kumi au zaidi wanaoweza kusaidia katika kazi hii maalum. (Muhimu: Kikundi kimoja cha watu wawili au watatu kinaweza kutumia mpango huu, lakini vikundi vingi vikifanya kazi wakati mmoja vinaweza kuleta matokeo mazuri zaidi).

Kila kikundi kitakuwa na wanaume wawili au watatu. Ni bora kama mmoja wa hao watatu katika kikundi atakuwa na ujuzi wa Biblia wa kutosha kuweza kuendesha mafunzo. Pia, kila kikundi kiwe na mtu mmoja anayejua lugha ya wenyeji vizuri zaidi. Atakisaidia kikundi kuelewa desturi za wenyeji. Kila kikundi kiwe na watu ambao ni Wakristo wanaoheshimika, wenye imani iliyoimarika na kukomaa. Wawe tayari kufanya kazi kwa majuma kadhaa, saa zisizopungua tano au sita kila siku.

Kujiandaa kirohoni na kuendelea kujiweka wakfu ni muhimu kwa watu hawa wanaokwenda kuanzisha makanisa mahali pengine. Vifundishe vikundi hivi kutenga nusu saa kila siku asubuhi na jioni kwa ajili ya maombi ya binafsi na kikundi, pamoja na kusoma Biblia. Hawawezi kuwagawia wengine wasicho nacho.

Fundisha umuhimu wa kuanzisha makanisa mengi madogo madogo, haraka. Vieleze vikundi hivi shabaha hii wazi wazi. Wafundishe kuwa tayari kwa matatizo katika uinjilisti na uanzishaji wa makanisa. Waruhusu kila mtu katika kila kikundi kujizoeza kufundisha.

Labda wanachama wa vikundi wanaweza kuishi katika nyumba za wale wanaotaka kuwavuta kwa Kristo na kuwafundisha. Lakini, labda itakulazimu kutoa hema, vitanda na vyombo vya kupikia. Mijini mnaweza kukodisha makao. Biblia na Agano Jipya, vitabu vya nyimbo, vikaratasi vya maelezo ya Biblia (tracts), masomo ya Biblia na mahubiri mafupi yanahitajika. Kila kitu kiwe katika lugha ya wenyeji wa eneo hilo. Biblia, Agano Jipya, vitabu vya nyimbo, n.k. viuzwe nusu ya bei ya dukani, au vitolewe bure, wakati kanisa linapoanzishwa. Mashine ya kunasa sauti na "cassette" zake zenye nyimbo, ushuhuda na masomo mafupi ya Biblia vitakuwa vya msaada.

## 2. Chunguza Mahali Pazuri pa Kuanzisha Mafunzo

Uchunguzi ufanywe majuma machache mapema katika maeneo ambayo vikundi vinatarajia kuingia. Watambue watu muhimu au wazee wa mahali hapo. Vijijini, jambo hili siyo gumu. Mjini, itakubidi kuuliza zaidi na kuwa mwangalifu. Waeleze wazee hawa juu ya hamu ya kuwaleta "waalimu wa Neno la Mungu" katika eneo lao. Eleza kwamba waalimu hawa watakaa kwa siku chache kuwasaidia watu kujua zaidi namna ya kumpendeza Mungu. Tafuta viongozi wa eneo hilo wanaoitikia wito. Jaribu kuomba msaada wa viongozi hao katika mpango mzima. Wanaweza kupendekeza mahali pa vikundi kula na kulala.

Baada ya uchunguzi na maandalio hayo kufanywa, chagua mahali pa kuanzisha mafunzo ya Biblia katika vijiji au maeneo. Ndipo, sasa, vikundi vitakuwa tayari kutumwa katika maeneo yao ya kwanza ya mji au vijiji.

## 3. Anzisha Mafunzo ya Biblia

Vipeleke vikundi kwenye eneo ulilochagua kuanzia. Tena, usisahau: ni lazima kikundi kiwaone viongozi au wazee wa eneo kwanza. Mpango wa mafunzo ya Biblia ni lazima uwe na yale yafuatayo:

Siku ya 1 __ Ushuhuda wa kila mshiriki katika kikundi, ukielekea kifungu cha Yohana 3:16
__ Mungu yu nani? (Tumia Biblia.)

Siku ya 2 __ Mwanadamu ni nani? (Endelea kutumia Biblia, na kuimba.)
__ Dhambi ni nini?
__ Kifo ni nini? - Cha mwili? Cha kiroho?

Siku ya 3 __ Yesu yu nani?

Siku ya 4 __ Kuzaliwa upya ni nini? Anza kutoa nafasi kwa watu "kumpokea Yesu na kuitii Biblia."

Siku ya 5 __ Kanisa ni nini?
__ Je, mngependa kuwa kanisa?
__ Kazi ya kanisa ni nini?
__ Endelea na makaribisho kwa watu kumpokea Kristo kuwa Mwokozi wao.

Siku ya 6 __ Nani anaweza kuliongoza kanisa?
__ Uwakili wa Kikristo ni nini?
__ Kanisa linategemezwa jinsi gani?
__ Endelea na makaribisho.

Siku ya 7 - 10
__ Nani anaweza kubatizwa?
__ Utakuaje kama Mkristo?
__ Utaijuaje Biblia?
__ Utaombaje?
__ Utashuhudiaje?
__ Endelea kukaribisha watu kumpokea Kristo, kutii Biblia, na kujiunga na kanisa.

Vikundi vikae hapo kwa siku nane hadi kumi. **Inawalazimu kuendelea kuwafundisha watu wale wale kila siku.** Watu wengine hawatahudhuria masomo yote, na wengine watajiunga wakiwa wamechelewa. Lakini mafundisho ya Biblia yaendelee kwa siku nane hadi kumi na watu wale wale. Vijijini mafunzo mengi yafanywe mchana watu wanapokuwa huru kuhudhuria. Mjini mafunzo mengine yanaweza kufanywa mchana na mengine jioni baada ya saa za kazi.

### 4. Anzisha Kanisa Jipya

Baada ya masomo "Yesu yu nani?" na "Kuzaliwa upya" (siku ya 4 hivi), toa nafasi kwa watu kumpokea Kristo. Uwe mwangalifu hapa. Usiwalazimishe watu katika uamuzi huu. Inawezekana watu wengi waliomo katika umati wataamua, "ndiyo tunamkubali Kristo na kuitii Biblia." Lakini, hakikisha kwamba kila mtu binafsi anakata shauri na kuelewa anachokifanya sawasawa. **Mkazo huu ni wa muhimu sana.**

Baada ya uamuzi huo kufanywa, kikundi kianze kufundisha kuhusu kanisa (somo la 5-9). Hakikisha watu wanaulizwa, "Je, mngependa kuwa kanisa?" Kwa uangalifu mwafundishe masomo hayo juu ya kanisa. Karibu na mwisho wa kipindi cha mafunzo, tafuta kuwaona wale waliookolewa. Fundisha kuhusu ubatizo na kukua katika Kristo. Ubatizo, kama ulivyofundishwa katika Agano Jipya, ni lazima utolewe kwa hao walioamini kuwa Yesu ni Bwana. Vikundi viwasaidie waliobatizwa kuwachagua watu watatu au wanne kuhudhuria masomo maalum kujifunza uongozi. Ndipo vikundi viondoke kuelekea kwenye maeneo yaliyo karibu kurudia mafundisho hayo hayo tena.

### 5. Wafunze Viongozi Wapya Katika Masomo Maalum

Siku chache zitakazofuatia ibada ya ubatizo, anza kuwafundisha viongozi wapya. Kikundi maalum cha waalimu wa Biblia kiwe tayari kuwafundisha viongozi hawa wapya siku nne. Wote wakusanyike mahali pamoja. Viongozi wapya wagharimie safari na kubeba sehemu ya chakula chao. Tena, wafundishwe jinsi ya kutumia Biblia, kuomba, jinsi ya kuwahudumia watu, na namna ya kuongoza na kuendesha ibada. Baada ya majuma matatu au manne, viongozi wapya wote hawana budi kujiunga na masomo ya Biblia ya TEE kwa mafunzo, au shule ndogo ya Biblia ianzishwe. Kama shule ya Biblia itaanzishwa, iendeshwe kwa siku nne au tano kwa mwezi. Mijini, mafunzo yanaweza kufundishwa saa za usiku na vitabu vya TEE vitumike. Ikiwezekana, tuma vikundi

kurudi na kutembelea makanisa hayo madogo mapya tena mara kwa mara.

Katika Mpango Wa Vikundi huu, hakikisha kuwa unaweka msingi imara wa kiroho. Kukua kwa makanisa kwa haraka kunaweza kutokea, mamia au hata maelfu ya watu wakiokolewa. Watahitaji wachungaji haraka sana; watahitaji mafunzo ya ki-Biblia.

Ikiwa waamini wapya hawapewi mafundisho mazuri wanayoweza kuyaelewa dhahiri, yawezekana warudie njia zao za zamani za dhambi. Au, labda watajaribu kuchanganya dhambi za zamani na njia zile mpya za kuishi Kikristo. Hawataimarika katika imani yao wala kanisa halitakua vizuri. Kwa hiyo, ni ya muhimu sana kugundua yule kiongozi wa kiroho Mungu anayemtaka kwa kanisa lile jipya. Huyo atajua shida za watu wake na atawatafutia msaada. Shida kadhaa ikionekana kuwa kubwa kuliko uwezo wake, atawaita wengine, pengine wanachama wa vikundi, waje kumsaidia kujua jinsi ya kufanya.

Katika kuanzisha makanisa mapya, kielelezo kizuri kinaonekana katika Waefeso 4:13: "...sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo."

Mtindo huu, MPANGO WA KUTUMIA VIKUNDI, ungefaa kutumika na wengi ulimwenguni kote. Jinsi mpango huu unavyoigwa na kutumiwa kwa makini, tuzidi kuomba: "Hatimaye, ndugu, twambeeni, Neno la Bwana liendelee, na kutukuzwa vile vile kama ilivyo kwenu" (II Wathesalonike 3:1).

Mpango wa Kutumia Vikundi ulianzishwa na
Clay Coursey, Malindi, Kenya.

# B. MPANGO WA KUSOMA MAANDIKO MATAKATIFU

Mpango huu umekwisha tumika Asia na Africa. Umebarikiwa na Mungu katika kutawanya Injili na uanzishaji wa makanisa. Kusoma Neno la Mungu kila siku katika nyumba nyingi, ndiyo kiini cha mpango huu. Hivi ndivyo mpango huu unavyofanya kazi:

**Sehemu ya 1: Chagua au Tayarisha Vifaa**

Nunua Agano Jipya zilizo katika lugha ya watu. Kama hii ni ghali, ama iwapo Agano Jipya hazipo, kijitabu chenye vifungu vya Biblia kinafaa. Au kitabu kifupi chenye hadithi za Agano la Kale na mafundisho ya maisha ya Yesu vitayarishwe. Kitabu hicho kiwe na vifungu vingi vya Biblia.

Pili, tayarisha "hati za makubaliano" kwa mamia. Ni lazima kuwa na nakala mbili za hati hizi kwa kila Agano Jipya au kitabu cha hadithi za Biblia ambacho kitatolewa. Hati hizo ziwe ifuatavyo:

TUNAKUBALI:

Tunakubali kusoma Kitabu Kitakatifu hiki kila siku. Ndiyo ________

Tunakubali kuwaita jamaa na marafiki kuja kusikiliza Kitabu hiki kikisomwa kila siku. Ndiyo ________

Tunakubali kutii Kitabu hiki Kitakatifu kila siku. Ndiyo ________

Jina: ______________________________

______________________________

**Sehemu ya 2: Nenda Kwenye Vijiji au Kwenye Nyumba**

Wafundishe wachungaji wengi au wazee wa kanisa waende vijijini au kwenye nyumba mijini. Wafunze kumtaka mkuu wa nyumba au mji. Wamwambie: "Tunataka kukupa Kitabu hiki Kitakatifu. Hili ni Neno la Mungu. Hatukiuzi; tunagawia wale wanaokubali kukisoma na kutii."

Kama mkuu huyo hawezi kusoma, mwambie: "Hata hivyo tunakupa wewe zawadi hii. Tafadhali wewe umchague au umtafute mtu fulani asome kitabu hiki kila siku. Na hakikisha unaiita jamaa yako na marafiki kusikiliza Kitabu hiki Kitakatifu kikisomwa kila siku."

**Sehemu ya 3: Onyesha Hati ya Makubaliano**

Unaweza kumwonyesha mkuu wa nyumba hati ya makubaliano wakati unapompa nakala ya Agano Jipya au kitabu cha hadithi za Biblia. Sema: "Tunatoa hati hii ili kujua kwamba umekubali kusoma na kutii hiki Kitabu Kitakatifu kila siku." Soma hati. Akikubali, vizuri! Weka alama penye "NDIYO" kwenye fomu. Unaweza kuandika jina lake na anwani, au anaweza kujaza hati hiyo mwenyewe. Mpe nakala ya hati kutunza ndani ya kitabu ulichompa, nawe utabaki na moja. Hii itamkumbusha alichokubali, na pia itakukumbusha wewe kuiombea jamaa hiyo na kutembelea nyumba hiyo tena.

Kama hataki kukubaliana na hati, hata hivyo yawezekana utataka kumwachia kitabu kile. Au pengine utamwachia kijitabu kidogo cha maandiko matakatifu ukimwahidi kuja baadaye na kumtembelea tena. Moyo wake unaweza kufunuliwa baadaye kwa mpango huu. Katika hali yoyote, onyesha urafiki na upendo wa Kristo.

**Sehemu ya 4: Rudi Pale Tena na Tena**

Andika ukumbusho ni mara ngapi umetembelea mahali. Usiwaharakishe kufikia uamuzi wa kuwa Wakristo. Lakini mweke Yesu moyoni mwako na katika mazungumzo.

**Mtegemee Roho Mtakatifu kulitumia Neno la Mungu katika kueleweshwa watu Habari Njema.**

Kama umetoa Agano Jipya, angalia wamesoma hadi wapi. Kama umetoa kitabu kidogo cha hadithi, pendekeza kwamba kitabu hicho kisomwe tena na tena, hata kama mara ya kwanza kilikwisha. Uliza na kujibu maswali.

## Sehemu ya 5: Usaidie Kikundi Kujiunga na Kuwa Kanisa

Kwa muda wa majuma au miezi kadhaa, kikundi kibaki kama "Ushirika wa kujisomea Neno." Hata hivyo, wanaweza kuongezeka au kukua kwa kuwakaribisha ndugu zao wengine zaidi, majirani, au marafiki. Ushirika huo ujengwe katika jamaa inayoongozwa na Kristo, chini ya mafundisho ya kila siku ya Neno la Mungu. Shabaha kuu iwe kuvuta jamaa nzima zote kwa imani ya Kristo (Matendo 16:31-34).


Usaidie watu hawa kuelewa jinsi ya kutubu na kumfuata Kristo. Jamaa nzima inaweza kutaka kukata shauri. Yawezekana kwamba jamaa nzima itataka kumpokea Kristo pamoja. Kila mmoja atampokea Kristo binafsi, lakini, pia wanaweza kuja kama jamaa.

Baada ya kikundi kukata shauri kumpokea Kristo, ueleze maana ya kanisa na kazi yake. Inawezekana kikundi kitapenda kujiunga na kanisa lililo karibu. Iwapo hivi ndivyo ilivyo, ni sawa. Kwa upande mwingine, kwa sababu ya umbali au sababu nyingine, watapenda kuwa na kanisa lao hapo. Ikiwa hivyo, wafundishe wajibu wa kanisa jipya: uinjilisti, kuabudu na kadhalika. Usaidie kikundi hicho kufikiria umuhimu wa muziki na sadaka. Ukaze mkazo juu ya mmoja wao kupata mafunzo ya uongozi kwa njia ya shule ya Biblia au TEE. Ufundishe kikundi kwamba kushirikiana na Wakristo wengine ni muhimu; kwa hiyo, kanisa jipya sharti liwe sehemu ya dhehebu la hapo.

Mwisho, ni vizuri kukumbuka kukieleza kikundi kwamba makanisa madogo yana faida nyingi. Kwa mfano: makanisa

madogo mapya yanazungukwa na "udugu" na uhusiano wao una nguvu. Makanisa madogo huwa na nafasi kwa kila mtu kushirikishwa. Mlinzi wa gereza pale Filipi alibatizwa "pamoja na jamaa yake...na alifurahi pamoja na nyumba yake nzima" (Matendo 16:33-34). Labda huu ulikuwa mwanzo wa kanisa dogo!

Mpango wa Kusoma Maandiko Matakatifu ulianzishwa na Dakt. Cal Guy wa Chuo cha Theologia cha Kibatisti kiitwacho "Southwestern Baptist Theological Seminary". Chuo hicho kiko Ft. Worth, Texas, Marekani. Mpango huu ulitungwa kutumiwa Bangladesh.



# KANISA LAKO LINAWEZA KUZAA!

# C. MPANGO WA KIKUNDI CHA URAFIKI



Mpango huu unaweza kutumika katika miji midogo na mikubwa, hasa katika sehemu ambazo ni vigumu kuvuta watu kwa Kristo. Mpango wa Kikundi cha Urafiki utasaidia katika sehemu ambazo makanisa hayajaanzishwa kwa sababu ya gharama kubwa ya ardhi.

**Hatua ya 1: Tafuta Viongozi wa Kujitolea**

Viongozi wawili wenye uwezo wanahitajika. Viongozi hawa watoke kwenye kanisa linalosaidia kazi hiyo mpya.

(A) **Mtu mmoja awe na ujuzi maalum** kama: jinsi ya kuishi na furaha mjini, jinsi ya kutafuta kazi nzuri, namna ya kuwa na nyumba ya Kikristo, namna ya kushinda hofu, jinsi ya kuimba vizuri, au namna ya kuwa na watoto wenye afya bora. Yeye anaweza kuwa na uwezo unaoweza kufundishwa kama: jinsi ya kupika chakula kizuri sana, kufundisha lugha ya Kifaransa au Kiingereza, kupiga gita, au mambo mengine ambayo watu wa mijini wanapenda kujifunza. Jaribu kujua mahitaji ya watu wa mijini ni nini. Mwalimu wa masomo haya ni lazima awe tayari kuja kufundisha mara 4 au zaidi.

(B) **Kiongozi wa pili yambidi kuwa na uwezo wa kufundisha Biblia.** Ni lazima awe tayari kuongoza majadiliano juu ya Biblia. Mtu mwenye ujuzi ama kipawa maalum na mwalimu wa Biblia anaweza kuwa mtu mmoja huyo huyo, kama anaweza kupatikana. Lakini mara nyingi itakubidi kuwapata watu wawili kwa kazi hizi mbili.

**Hatua ya 2: Tafuta Nyumba au Mahali Pengine pa Kukutania**

Tafuta nyumba ambayo mume hakatai kikundi kukutana mara moja kwa juma nyumbani mwake. Nyumba ambayo wote mume na mke ni Wakristo wapya ni bora zaidi. Mahali pa kukutanikia ni lazima pawe pale pale na wakati ule ule kila juma.

Sehemu nyingine za kukutanikia zinaweza kupatikana kama: jengo la umma, katika ukumbi wa mikutano hotelini, madukani na shuleni.

**Hatua ya 3: Wakaribishe Watu**

Jambo hili lifanyike katika njia mbili:

(A) Kwa kuweka matangazo katika mahali palipo watu wengi. Fuata mfano huu:

MNAKARIBISHWA

**Karibuni kujifunza** (kutafuta kazi nzuri, au kuzungumza Kiingereza, n.k.)

**Karibuni kujifunza Biblia**

Mahali: (Maelezo ya pale nyumba ilipo) au ramani.

Tarehe: Kila Jumapili, kuanzia Nov. 11

Wakati: Saa 10 jioni hadi saa 11:30

Karibuni kujifunza! Njoo No. 11, Saa 10 jioni!

Kwa maelezo zaidi, mwulize Mary Mbathi

Simu 7061, au Box 3021, NAIROBI

(B) Kuwakaribisha watu pia kunaweza kufanyika kwa kutembelea nyumba kwa nyumba. Waambie watu kilichopangwa. Waeleze masomo yale mawili yatakayofundishwa. Eleza waziwazi kuwa Biblia ni somo mojawapo litakalofundishwa. Mweleze kila mmoja mahali pa mkutano, tarehe na wakati.

**Hatua ya 4: Fundisha Vizuri**

Timiza ahadi yako ya kufundisha "Jinsi ya....". Hakikisha kwamba watu wanajifunza kitu kipya, tena ni kitu wanachokihitaji katika maisha ya mijini. Usijaribu kufundisha kila kitu katika mkutano mmoja. Panga ili mafundisho yaendelee mara nne au zaidi.

Waambie watu ya kuwa mikutano hiyo inaendeshwa kwa sababu ya upendo wa Kikristo. Weka wakati wa kujifunza Biblia katika kila mkutano. Wakati wa kujifunza "jinsi ya..." na wakati wa somo la Biblia uwe dakika 30-40 kila moja. Mwalimu wa Biblia atayarishe majadiliano yanayolenga shida za kimaisha kama: huzuni (Warumi 8:38-39), ugonjwa (Zaburi

6:2-4) na shida za jamaa (Waefeso 5:21-6:4). Masomo mengine yanaweza kutoka katika vitabu vya Biblia kama Marko au Yohana, au juu ya wanaume na wanawake wenye sifa nyingi katika Biblia.

Fundisha vizuri kuhusu Kristo. Ni lazima watu wajue vya kutosha ili waweze kuamua kuwa wafuasi wa Kristo. Fundisha jinsi Yesu anavyotaka kuwaweka watu huru. Fundisha jinsi Yesu anavyotoa nguvu kuu zake zinazoweza kushinda dhambi, mapepo machafu, ugonjwa na kifo. Anza na yale ambayo watu wanapenda na kuhitaji, na endelea kutoa Neno la Mungu kwao ili liwaeleze jinsi walivyo.

Endelea na mikutano hiyo kila juma. Ikiwepo nafasi ya kutosha mnapokutana, wakaribishe watu wengine. Masomo juu ya "jinsi ya..." yatakapomalizika, jaribu kuendelea na masomo ya Biblia kwa wale wote watakao kubali. Hii ni muhimu zaidi. Hadi hapa, ulichokifanya kinaweza kuwa msingi mzuri wa kanisa jipya.

**Hatua ya 5: Karibisha Watu Kumkiri Kristo**

Wakati masomo ya Biblia yanapoendelea, eleza jinsi mtu anavyoweza kuwa Mkristo. Hali inaporuhusu, karibisha watu kumpokea Kristo. Fundisha juu ya ukuu wa Kristo na hakikisho la wokovu. Watu wanapookolewa, zungumzia kujiunga na kuwa kanisa, kupata ubatizo, n.k. Usichelewe kuliita kundi hilo jipya "kanisa." Makosa hufanyika hapa kwa kushindwa kukubali kwamba kundi dogo la waamini wapya linaweza kuitwa kanisa.

Kanisa ni kundi la waamini waliobatizwa, hata wakiwa 10 au 12, ambao wamejiunga pamoja kama Agano Jipya linavyoagiza kumwabudu Mungu na kupanua ufalme wa Kristo.

Jadili kuhusu uwezekano wa kuwa na ibada katika nyumba za washiriki, kama kanisa changa. Epukana na shida za mikutano ya kinyumbani. Hii inawezekana kwa kukubali

kukutana kwa vikundi vidogo vidogo, badala ya kujazana kiasi kwamba jengo lenye gharama lihitajike. Mara nafasi kubwa kuliko nyumba inapohitajika, pengine majawabu ya shida hii ni:

(A) Gawanyikeni katika vikundi vidogo vidogo kwa baadhi ya mikutano.
(B) Kodisheni chumba kikubwa zaidi.
(C) Kama vikundi kadhaa vitakua na kuwa na nguvu za kutosha, fikiria juu ya kushirikiana pamoja na kununua ardhi na kujenga hapo.

Mwanzo wa Mpango wa Kikundi cha Urafiki ulizinduliwa na Dakt. Ralph Neighbor kwa matumizi huko Singapore.

# III
# MIPANGO MIFUPI YA KUANZISHA MAKANISA MAPYA

Sasa umekwisha zifahamu hatua muhimu kuhusu namna ya kuanzisha kanisa. Ifuatayo ni mipango mifupi mingine kwa kuanzisha makanisa mapya. Mitindo yenyewe ilikusanywa kutoka sehemu mbalimbali za dunia. Mungu amekwisha bariki mipango hii wakati walikuwa Wakristo waaminifu walikuwa wakifanya kazi yake kuwaleta wengine kwa Kristo. Ongeza mambo mengine kutokana na ujuzi wako mwenyewe au kufuatana na mipango mingine mirefu iliyotolewa mbele katika kitabu hiki.

## Mpango Mfupi wa 1: Kuanzisha Makanisa na Muziki

Anzisha kanisa jipya kwa jitihada za muziki. Mpango huu unasaidia katika miji mikubwa na sehemu ambazo wasio Wakristo wanao uvuto. Inahitaji kujitoa hasa, wakati, na vipawa vya kikundi cha waimbaji. Kuanzia kanisa kwa jitihada za muziki:

(A) Mtafute kiongozi mwenye kipawa cha muziki tena anayewapenda wapotevu.

(B) Anza kutafuta vikundi vya waimbaji wa kwaya. Hakuna haja ya kwaya kubwa, lakini muziki mzuri utakuwa wa lazima.

(C) Tafuta mahali pa kuwa na jitihada ya muziki. Pawe karibu na pale ambapo makanisa mapya yanatarajiwa kuanzishwa, na mahali ambapo watu huweza kufika rahisi.

(D) Tembelea nyumba za watu. Tangaza mikutano katika magazeti, n.k.

(E) Tayarisha nyumba kadhaa ambako masomo ya Biblia yanaweza kuendeshwa. Wapate waalimu wa masomo haya.

(F) Anza mikutano ya saa moja mzima ya muziki, ikifuatiwa na matangazo kuhusu vikundi vya masomo ya Biblia. Endelea na muziki kila usiku. Waimbaji wanalazimika kufahamiana na watu wanaohudhuria. Wawe wanawakaribisha kwenye mikutano ya masomo ya Biblia.

(G) Endelea na mpango huu wa muziki kama majuma mawili hivi. Kutembelea na masomo ya Biblia katika nyumba viendelee kwa miezi kadhaa.

Kwa njia ya mchanganyiko huu wa muziki, kutembelea, na masomo ya Biblia, makanisa yanaweza kuanzishwa kutokana na wale wanaomkiri Kristo kuwa Mwokozi. Mpango huu wa muziki utumike kwenye maeneo mengine ya mji ule kusaidia uanzishaji wa makanisa huko.

# Mpango Mfupi wa 2: Kuanzisha Makanisa na Wanafunzi

Anzisha kanisa na wanafunzi wa shule ya sekondari au chuo kikuu. Vijana Wakristo wawili au watatu ambao wamejitoa hasa wanaweza kuanzisha kanisa. Ni lazima wawe radhi kutoa wakati wao wa zaidi kwa kuzitembelea nyumba, na kuendesha masomo ya Biblia pamoja na kuongoza muziki. Kazi hizi zitafanywa baadaye na watakaoamini kuwa washiriki wa kanisa jipya.

Wanafunzi wanaweza kutumia mpango mmoja kati ya ile iliyotajwa mapema katika kitabu hiki. Lakini mambo mawili ya lazima yatahitajika:

(A) Kuanzisha na kikundi kidogo, ambacho —
(B) Kitaanza kusoma Neno la Mungu pamoja.

Baada ya matayarisho ya kiroho ya maombi na kupatikana kwa mahali pa kukutanika, wanafunzi waanze kutembelea nyumba za watu. Hapo watasoma vifungu, wataimba, wataomba na kuwakaribisha watu kwenye mikutano.

Wajaribu kuwavuta watu wa kila umri, na sio wanafunzi wenzao tu. Hili linaweza kufanyika kwa kuwaomba wazee kadhaa katika eneo wanalotembelea kutembelea pamoja nao. Pia waamini wapya ambao wamekomaa kidogo kirohoni washirikishwe katika shughuli wanazozifanya vijana hao ili wapate ujuzi wa kuongoza ibada.



# Mpango Mfupi wa 3: Kuanzisha Makanisa Na Mahitaji ya Maombi


Kuna njia mbili ambazo uwezo wa maombi umetoa msaada katika kuanzisha makanisa mapya. Mfano mmoja ni ule wa kanisa la Kathemboni, Kenya. Baada ya Injili kutokewa wazi, watu wachache walimpokea Kristo kuwa Mwokozi. Ndipo Bwana Kamuti aliwasihi hao waliookolewa kuandika majina ya ndugu zao ambao bado hawajaokolewa kwenye vikaratasi. Kwa wakati fulani maombi yalitolewa kwa ajili ya hao ndugu wapotevu. Kisha majina hayo yaligawanywa kati ya Wakristo, ambao walikwenda kuwatembelea na kuwashuhudia ndugu hao wapotevu. Kwa kuchanganya maombi na ushuhuda moja kwa moja kwa jamaa, watu wengine zaidi waliokolewa. Kwa njia hii kanisa lenye nguvu lilianzishwa.

Mfano mwingine wa makanisa yaliyoanzishwa kwa njia ya mahitaji ya maombi upo Rosario, huko Argentina. Mchungaji Bruno, huko, alifundisha washiriki wake kwenda katika kila nyumba na kuwaambia watu ya kuwa kama wana shida, wao wataziombea. Mahitaji ya maombi yaliyo wazi kuhusu kazi, watoto, wokovu, kuponywa na kadhalika yalichukuliwa na kurudishwa kwenye kanisa na kuombewa. Majina, anwani, mahitaji ya maombi na siku yalipojibiwa vilitunzwa kwa makini. Maombi yanapojibiwa na Bwana, watu wako tayari kusikiliza Injili! Kisha mikutano ya uinjilisti inafanyika na vikundi vya kusoma Biblia vinaanzishwa, kutembelea kunaendelea na makanisa mapya yanazaliwa. Washiriki wa makanisa hayo machanga, hasa, ni wale ambao maombi yao yalijibiwa.



# Mpango Mfupi wa 4: Kuanzisha Makanisa na Ramani

Utumiaji kwa uangalifu wa ramani umesaidia sana uanzishaji wa makanisa mapya. Kwanza, ikiwezekana nunua ramani zilizo nzuri za mahali yanapohitajika makanisa mapya. Pili, ukitumia ramani ulizonunua au ufahamu wako binafsi wa mahali hapo, **uchore ramani.** Chora ramani ambazo zinazoonyesha habari itakayotumiwa katika kuamua makanisa mapya yanaohitaji wapi. Tazama mfano unaofuata hapa:



Baada ya ramani kama hiyo juu kutengenezwa, **angalia sehemu zilizo wazi.** Katika mfano huu tumeweka alama za swali (?) katika sehemu zilizo wazi. Haya ndiyo maeneo yanaohitaji kuchunguzwa kwa uangalifu ili ujue ikiwa kuna nafasi na mahitaji kwa kanisa jipya hapo. Kwa vyovyote, inakubidi kupeleleza wingi wa watu, mahali shule zilipo, na kadhalika. Unaweza kutumia mpango wa namna yoyote uliopo katika kitabu hiki katika kuwavuta watu kwa Kristo na kuanza makanisa mapya.

Hata hivyo, kwenye maeneo uliyochagua kuanzisha makanisa mapya, WEKA MBELE KUTEMBELEA NYUMBA. Uchunguzi uliofanywa Afrika Mashariki na makanisa ya Kibatisti unaonyesha kwamba kutembelea nyumba kwa nyumba ndio mtindo uliotumika katika kuanzisha 63% ya makanisa mapya yote. Inaonekana na viongozi wa makanisa ya kuwa kutembelea na kushuhudia vinafaa kuliko kuhubiri katika kuwavuta watu kwa Kristo. Kuona maeneo yenye mahitaji, kwa njia ya ramani, kisha kutembelea jamaa moja-moja, kutasaidia makanisa mapya kuzaliwa.

# Mpango Mfupi wa 5: Kuanzisha Makanisa Kwa Vifaa Vya Maonyesho

Makanisa yanaweza kuanzishwa kwa matumizi mazuri ya vyombo vya maonyesho. Injili ikitangazwa kwa njia hii, watu watasikiliza. Kisha wazo la kuwa na kanisa litaanza kukua katika mawazo yao. Ikiwezekana, pamoja na vifaa vya maonyesho vinavyotajwa hapa chini, tawanya makaratasi yaliyo na picha chache zilizokuwa katika maonyesho. Zifuatazo ni njia nne za kutumia maonyesho:

(A) **Tayarisha picha za "slides"** zinazoonyesha jinsi jamaa fulani ilivyompokea Kristo. Au tayarisha "slides" kuonyesha jinsi kundi la watu 50-100 walivyookolewa katika eneo moja, au jinsi kanisa moja dogo lilivyoanzishwa. Nunua mashine za "slides" zinatumia mawe, yaani battery. (Mfano wa kampuni inayouza mashine za namna hii ni: Mitchell Art Productions, 4435 W. 58th Place, Los Angeles, California 90043, U.S.A.) Onyesha picha mashuleni, majumbani, na sokoni, mahali ambapo kanisa jipya linahitajika. Ni lazima urudi tena na tena mahali pale pale na kuwatembelea watu nyumba kwa nyumba.

**Nunua picha Kibiblia za Biblia.** Hizi hupatikana zikiwa moja moja au katika "seti." Wafundishe wasaidizi wako hadithi nane au kumi zinazoelezea picha hizo. Wapeleke wasaidizi hao kwenye eneo linalohitaji kanisa jipya, ili wasimulie hadithi za Biblia katika kila nyumba. Warudie kutembelea nyumba hizo mpaka watakapokuwa wamesimulia hadithi za picha zote. Picha kubwa za kibiblia, nyingine zikiwa zimechorwa na Waafrika, zinapatikana katika maduka ya vitabu vya Kikristo. (Maduka ya Kikatoliki yanayo seti moja ya picha zilizo na rangi nzuri ambazo zilichorwa na mchoraji C. D. Mawa.)

(C) **Mikanda ya sinema yaani "Filmstrips"** imetumika kusaidia kuanzia makanisa mapya. (Angalia anwani ya Mitchell Art Productions juu). Madhehebu kadhaa hapa Afrika, kama Baptisti, yanatayarisha mikanda ya sinema na "wachezaji" Waafrika. Hizi zaweza kununuliwa kutoka kwa Zeb Moss, Box 48390, Nairobi, Kenya. Visa vinavyopatikana ni "Maisha ya Kikristo", "Vijana", "Utunzaji wa Watoto", na "Ulishaji Mzuri."

(D) **Sinema** pia zimesaidia kutayarisha mahali pa kuanzisha kanisa. Sinema yenye hadithi za Biblia ni bora zaidi. Sinema za Kikristo zinaweza kukodishwa kutoka kwa vyama mbalimbali kama National Christian Council, Life Ministries, Afromedia, na vyama vingine vya kanisa.

Vifaa hivi vya maonyesho vinasaidia kuleta mvuto kwa watu wanaoishi mahali fulani. Hata hivyo, inakubidi kufuatia mvuto huo na mambo mengine yaliyo katika "Mpango Maalum wa Kimsingi."

# Mpango Mfupi wa 6: Kuanzisha Makanisa Na Mashine za Kunasa Sauti

Inakulazimu kununua mashine za kunasa sauti. Katika lugha wanayosikia wenyeji, nasa **hadithi** kama zifuatazo:

(A) Hadithi katika nyimbo-ikiwezekana, nyimbo hizo ziwe katika sauti ya nyimbo za kienyeji.

(B) Hadithi za asili kama vile hadithi za Esopo au hadithi za wanyama. Tafuta hadithi za namna hii zitakazoeleza mafundisho ya Biblia.

(C) Hadithi za kweli kuhusu watu ambao wameokolewa, au ushuhuda wa watu binafsi.

(D) Hadithi za kweli zinazoeleza maombi yaliyojibiwa.

(E) Hadithi za Biblia katika Agano la Kale zinazolinganisha na desturi za wenyeji, na hadithi za Agano Jipya kueleza Habari Njema.

Hadithi hizi zinaswe katika mikanda ya kaseti minne au mitano. Maeneo yanayohitaji makanisa mapya yachaguliwe, na wachungaji au wasaidizi wake wapewe mashine ya kunasa sauti. Watu hawa warudi tena na tena kwenye jamaa wanazozitembelea hadi hapo mikanda ya kaseti yote itakapokuwa imesikiwa. Baada ya mikanda hiyo kusikiwa, vikaratasi vinavyoeleza hadithi zile zile vitasaidia sana, vikitawanywa kwa jamaa zile. Kufuatilia kwa mpango huu wa kuanzisha makanisa na matumizi ya mashine na kunasa sauti kunahitajika. Kwa hiyo, angalia tena ule Mpango Maalum wa Kimsingi wa kuanzisha makanisa.

# "MOTO WAKO UJE!"

**"Nimekuja kutupa moto duniani; na ukiwa umekwisha washwa, ni nini nitakalo zaidi?" Luka 12:49.**

Kristo aliposema "Nitalijenga kanisa langu," shabaha yake ilikuwa kubadilisha ulimwengu. Alikuja kuleta "moto" juu ya nchi. Kristo anapenda kanisa lake lisambae kama moto ulioshika pori. Anataka ulimwengu ubadilishwe kwa moto wa mapinduzi yake.

Katika kitabu hiki, tumejihusisha na mawazo, mipango na mitindo mipya. Kufuatana na ulimwengu ulivyo sasa, kwa kweli tunahitaji mawazo na mipango mipya. Tunatafuta njia mpya kwa siku mpya. Tunatamani Mungu kutupatia BUSARA YAKE ili tujue jinsi ya kuanzisha makanisa mapya mengi.

Na bado......tunalia:
"Moto wako uje!"

Kwani tukiwa na busara ya kujua jinsi ya kufanya kazi yake, tunaitia NGUVU YA KIROHO. Yohana aliahidi kwamba, "Yesu atawabatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa moto" (Luka 3:16). Kwa kweli, mioyo yetu inalia kwa sauti leo, "Moto wako uje!"

Moto ulipoanguka mlimani Karmeli ilikuwa ishara ya UTUKUFU WA MUNGU kuwepo. Elisha alipoyaona magari ya moto, yalikuwa ishara ya ULINZI WA MUNGU. Na leo tunaomba: "Eh, Bwana, moto wako uje!"

Siku ya Pentekoste, ndimi za moto za Roho Mtakatifu ziliwafanya wawe na bidii, huruma na upendo. Leo mipango yetu inabaki tupu bila vile bidii, huruma na upendo. Na hivyo, mioyo yetu inalia tena, "Eh, Bwana, ulete moto wako!"

Na tuombe! "Eh, Bwana Mungu, haya ndiyo tunayohitaji - ule moto mpya wa utukufu, bidii na upendo wako. Tunahitaji busara na mipango na njia za kazi. Tunahitaji mawazo na maelezo mapya. Lakini, mioyo yetu inalilia kuwa moto wako uwake tena katika maisha yetu! Na Roho wako awe juu yetu, atusafishe, atuwezeshe na atufundishe! Twaomba moto wako uje juu yetu! Eh, Bwana Mungu wetu, moto wako uje!

Katika jina la Yesu Mwokozi wa ulimwengu,
Amin!"

# NYONGEZA:

## KAZI KUFANYIKA KUSAIDIA KUJIFUNZA

Kama unatumia kitabu hiki katika mkutano wa kukuza kwa kanisa, zifuatazo ni kazi zitakazo kusaidia kuelewa yaliyo katika kitabu hiki. Hata kama unajisomea binafsi, unaweza kuzitumia nyingi za kazi hizi za kujifunzia. Mabadiliko hutokea katika maarifa, tabia na uwezo wetu tunapojihusisha na mambo ambayo tunaelekezwa tunaposoma. Jibu maswali na fanya kazi hizo, hivyo utayafanya mafunzo yako kudumu na utaonyesha kwa vitendo ufahamu wako wa jinsi ya kuanzisha makanisa.

1. **Kutoka kwenye utangulizi,** ukurasa 1.

   A. **Katika utangulizi, tafuta hadithi tatu kuhusu makanisa yanayoanzishwa haraka. Kutokana na hadithi hizi, jaza kwa namba ya ongezeko katika kila eneo. Kwa mfano,**

      1. **Katika wilaya moja huko Kenya, kulikuwa na ongezeko la makanisa kuanzia [5] hadi [65].**

      2. **Mfanya kazi katika kiwanda alianzisha kanisa; sasa kuna makanisa [ ] katika eneo lile.**

      3. **Mwalimu mmoja alizindua mpango, na makanisa zaidi ya [ ] yalianzishwa, na watu zaidi ya [ ] waliokolewa.**

B. Andika maana ya neno "kanisa." ____________________

________________________________________

________________________________________

C. Katika maneno yako mwenyewe, au maneno ya Biblia, eleza sababu nne kwa nini unafikiri makanisa mapya zaidi yanahitajika.

1. ________________________________________


2. ________________________________________

3. ________________________________________

4. ________________________________________

2. **Kutoka kwenye: Mpango Maalum wa Kimsingi, ukurasa 11.**

A. Soma yaliyo katika ukurasa 11 kwa uangalifu, ukirudia hadi "hatua saba katika kuanzisha makanisa" mara nyingi. Sasa kwa njia ya kumbukumbu, bila kutazama nyuma, jaza nafasi zilizoachwa hapa:



3. **Kutoka hatua ya 1: Panga na omba,** ukurasa 12.

A. Kwa kutumia karatasi tofauti, andika kwa kifupi vile ungewaambia washiriki wa kanisa lako, ukiwatia moyo wazidi kuomba kuhusu kuanzisha kanisa jipya.

B. Zungushia maneno manne yanayoonyesha jinsi Yesu alivyotayarisha mipango yake:
Mathayo 9:35: "Naye Yesu alikuwa akizunguka katika miji yote na vijiji, akifundisha, katika masinagogi yao, na kuihubiri Habari Njema ya ufalme, na kuponya magonjwa yote na udhaifu wa kila aina."

4. **Kutoka hatua ya 2: Tafuta Wasaidizi,** ukurasa 14.

A. Soma mambo matano muhimu kwa watu utakaowaweka kukusaidia. Angalia vifungu vitano vilivyotolewa (II Timotheo 1:12, n.k.). Andika mambo mawili ambayo unayafikiria kuwa muhimu zaidi katika maisha ya wale wanaoanzisha makanisa.

1. ______________________________

2. ______________________________

B. Kwa kutumia karatasi tofauti, mwandikie barua mtu fulani kanisani kwako, ukimsihi akusaidie kuanzisha kanisa. Mwambie kwa nini unafikiri anafaa, na kiasi ambacho kitabu unachosoma kinaweza kumsaidia.

5. **Kutoka hatua ya 3: Chunguza Maeneo,** ukurasa 16.

A. Ili kufanikisha uchunguzi, ni mambo gani mawili yanahitajika?

1. ____________________

2. ____________________

B. Chagua mtu fulani ajifanye yuko kazini nawe. Jifanye umefika katika eneo fulani na unauliza yale maswali 12. Zifanye fikira zako za makisio kwamba upo kwenye eneo, katika mtindo wa kikweli.

C. Iwapo mahali mnaposoma mafunzo patakuruhusu, uende kwenye eneo lililo karibu, na fanyeni uchunguzi, mkitumia yale maswali 12.

D. Tayarisha taarifa fupi ambayo ungeweza kutoa kama ripoti kanisani, ukiwaeleza wazee ulichogundua katika uchunguzi. Toa mapendekezo yako ukitoa sababu, kanisa jipya lianzishwe katika eneo fulani.

6. **Kutoka hatua ya 4: Tembelea Jamaa,** ukurasa 20

A. Orodhesha mambo matatu ya kuzungumzwa utakapotembelea jamaa.

1)____________ 2)____________ 3)____________

B. Kwa njia ya maigizo, chezeni mchezo juu ya kutembelea jamaa moja kwa njia nzuri. Pia, labda utapenda kucheza ukionyesha kutembelea jamaa katika njia mbaya.

7. **Kutoka hatua ya 5: Tafuta Mahali pa Kukutanikia,** ukurasa 24

A. Orodhesha sehemu sita ambazo kanisa linaweza kuanzishwa.

1. ____________________

2. ____________________

3. ____________________

4. ____________________

5. ______________________________

6. ______________________________

B. Kutokana na ujuzi wako mwenyewe, toa mifano ya kanisa jipya linaloanzishwa katika maeneo haya.

8. **Kutoka hatua 6: Anzisha Mikutano, ukurasa 27.**

A. Ni namna zipi mbili za mikutano zenye msaada katika kuanzisha kanisa?

1. ______________________________

2. ______________________________

B. Soma orodha ya mapendekezo kumi ya mikutano ya kujisomea Biblia. Kutokana na orodha hiyo, chagua mambo matatu ambayo kwako yanaonekana muhimu zaidi.

1. ______________________________

2. ______________________________

3. ______________________________

C. Wahoji watu wanne, ukiwauliza: "Je, unafikiri ni muhimu kumwabudu Mungu? Kwa nini kumwomba Mungu ni muhimu?"

D. Soma kwa uangalifu mpango uliotolewa kwa ibada ya kanisa jipya. Ni kwa njia zipi ungebadilisha mpango huu? ______________________________

9. **Kutoka hatua ya 7: Mtafute na Kumfundisha Kiongozi, Ukurasa 32.**

A. Andika mambo matatu uliyojifunza kuhusu kiongozi anayefaa.

1. ______________________________

2. ______________________________

3. ______________________________

B. Soma vizuri mambo matano kuhusu mwito wa Mungu, ukisoma katika Biblia yako vifungu vyote ulivyopewa (Mathayo 23:8-12, n.k.).

C. Eleza vile unaweza kumsaidia mchungaji mpya kuweza "kujilisha" mwenyewe kiroho.

______________________________

______________________________

10. **Kutoka kwenye: Mipango Mingine kwa Kuanzisha Makanisa,** ukurasa 38.

A. Chunguza mchoro unaoonyesha vipindi vya ukuzi wa kanisa. Fupisha vipindi hivi kwa maneno yako mwenyewe.

B. Eleza kwa nini unakubali au kuupinga mchoro huo.

11. **Kutoka kwenye: Mpango wa Kutumia Vikundi, ukurasa 40.**

A. **Katika karatasi nyingine, andika ili mikazo mitano muhimu kutoka kwenye Mpango wa Kutumia Vikundi, ukiipanga kihatua. Zungushia maneno muhimu katika kila njia ya hayo mikazo mitano.**

B. **Mwandikie barua mchungaji mwenzio, ukimwambia juu ya mpango huu wa vikundi. Msihi mchungaji huyo ajiunge nawe katika matayarisho ya kutumia mpango huu katika kuanzisha makanisa mapya.**

12. **Kutoka kwenye: Mpango wa Kusoma Maandiko Matakatifu**, ukurasa 46.

A. Soma mpango huu kwa uangalifu, hasa sehemu tano za mpango huo. Kwa kufikiria hali yako mwenyewe, eleza kwa nini unafikiri mpango huo utafaulu au kushindwa katika eneo lako.

B. Soma Matendo 16:25-34 katika Biblia yako, kisha jibu maswali yafuatayo:

1. Ni nini Paulo na Sila walichokitumia kama kisa cha mazungumzo kwa jamaa? (kifungu 32) ______

______________________________

2. Matokeo ya mara moja baada ya kuokolewa kwa jamaa hizi yalikuwa yapi? (vifungu 33-34) ______

______________________________

C. **Fanya maigizo kwenye sehemu mbili:**

1. **Kufika katika kijiji au nyumba mjini, fanya sehemu ya 2 na 3.**

2. **Ukirudi tena kijijini au kwenye nyumba mjini, jadiliana na kundi au jamaa kuhusu sehemu ya 5: Kujiunga na kuwa kanisa.**

D. **Unga mkono kwamba "Makanisa Madogo yana faida nyingi." Orodhesha faida zilizotolewa katika kitabu hiki na uongeze sababu zako mwenyewe.**

1. ______________________________

2. ______________________________


3. ______________________________

4. ______________________________

5. ______________________________

13. **Kutoka kwenye: Mpango wa Kikundi cha Urafiki,** ukurasa 50.

A. Pambanua njia tano za mpango huu. Unaweza kufanya hivyo kwa kutumia "Chati" ifuatayo. Jaza nafasi zote. Kisha mweleze rafiki yako juu ya mpango huu — Kikundi cha Urafiki, ukimwonyesha chati hii.




B. Nenda, ukazungumze na watu watatu ambao wanaweza kufaa katika kikundi cha urafiki. Waulize mawazo yao: wanafikiri watu wa mjini wangependa kujifunza nini? Pendekeza uwezekano kama ilivyoandikwa katika hatua 1, A.

14. **Kutoka kwenye: Mipango Mifupi ya Kuanzisha Makanisa,** ukurasa 55.

A. Soma kwa sauti mpango mfupi wa kwanza: "Kuanzisha na Muziki." Unaposoma, jaribu kutambua mambo saba (A-G) yaliyo muhimu katika mpango huu. Kisha jadili faida za kuwa na mpango wa muziki katika eneo lako.

B. Baada ya kusoma kwa uangalifu mpango mfupi wa pili, fikiria kama inawezekana kwenda kwenye chuo au shule ya sekondari iliyo karibu. Tayarisha mazungumzo ya Chama cha Wakristo hapo au wanafunzi wa dhehebu lako, kuhusu vikundi vya wanafunzi kuanzisha makanisa mapya madogo.

C. Soma mifano miwili iliyotolewa katika mpango mfupi wa tatu: "Kuanzisha na Mahitaji ya Maombi", kisha mwe na jadiliano juu ya kuanzisha makanisa kwa mpango huu wa mahitaji ya maombi.

D. Baada ya kusoma mpango mfupi wa nne, tayarisha ramani ya eneo lako. Kwa kuangalia sehemu zilizo **tupu** katika ramani, amua ambako makanisa mapya yanaweza kuhitajika. Kisha tayarisha hatua za uchunguzi zikifuatiwa na kutembelea nyumba kwa nyumba katika sehemu hizo.

E. Soma kwa sauti vile vifaa vinne vya maonyesho katika mpango mfupi wa tano. Usihi kikundi kusikiliza kwa makini, kama kuna mawazo yanayoweza kufaulu katika mazingira yao. Kisha jadiliana juu ya kutumia moja ya vifaa hivyo vya maonyesho kuanzisha kanisa jipya.

F. Mwandikie Mmisheni barua, ukimwambia juu ya mpango mfupi wa sita: "Kuanzisha na Mashine ya Kunasa Sauti." Mwombe mmisheni kuja kanisani kwako ili wazungumzane juu ya kunasa zile nyimbo na hadithi, na kutumia mashine ya kunasa sauti kusaidia uanzishaji wa makanisa mapya.

15. **Kutoka "Moto Wako Uje!"**, ukurasa 65.

A. Mchague mtu mmoja kusoma kwa sauti mbele ya darasa, "Moto wako uje!" Waombe kikundi hicho kusikiliza maneno hayo wakiwa wameinamisha vichwa katika maombi, kila mmoja akifikiria juu ya eneo lake lenyewe na mahitaji yake.

B. Funga mkiwa na majira ya maombi, huku kila aliyeshiriki katika masomo hayo, akiomba juu ya umuhimu wa kwenda na kuanzisha makanisa mapya mengi, na mengi, na mengi.....kwa ajili ya Kristo.